
BFAM

SWAHILI www.iBFAM.org

KUZAA NA KUONGEZEKA +

# KUGUNDUA SIRI ZILIZOFICHIKA KATIKA BIBLIA

ANZA KUISHI MAISHA YA UTELE AMBAYO MUNGU ALIYAPANGA KWA AJILI YAKO



## CHOMBO CHA KUJIFUNZA BIBLIA KWA VITENDO NA MITAALA

*ITAKAYOFUNGUA SIRI ZILIZO KATIKA BIBLIA*

*“Hayo yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, nitafumbua kinywa changu kwa mifano, nitayatamka yaliyositirika tangu awali.” (MATHAYO 13:34-35)*

# BE FRUITFUL AND MULTIPLY

A PRACTICAL BIBLE STUDY TOOL AND CURRICULUM

BFAM MANUAL + THE ESSENTIALS SERIES

Published by:
Every Home for Christ International
P.O. Box 64000, Colorado Springs, CO 80962-4000 USA
(719)-260-8888
BFAM@ehc.org
www.iBFAM.org

Copyright © 2012 by Every Home for Christ

Permission is granted to reproduce and distribute this material provided that:

- Proper credit is given to the author - Every Home for Christ International.
- Every Home for Christ is notified of where and how materials are being used.
- It is not sold for a fee beyond the cost of duplication.

Translations and adaptations for context are encouraged provided that:

- Translations are coordinated through Every Home for Christ International.
- An agreement has been made to recognize Every Home for Christ as the copyright owner of all translations and versions.
- All adaptations in content are approved by Every Home for Christ.
- A final copy is provided to Every Home for Christ for archive and distribution purposes (preferably a printed and a digital copy.)

BFAM lessons are based on a discipleship method that must be understood in order to receive maximum benefit from each lesson. If you have not received specific training on how to use BFAM, please contact Every Home for Christ.

All Scripture quotations, unless otherwise indicated, are from the TODAY'S NEW INTERNATIONAL VERSION®, TNIV®. Copyright © by International Bible Society. Used by permission of Zondervan Bible Publishers. All rights reserved.

Distributed by Every Home for Christ International

# BFAM Yaliyomo

## KITABU KINACHOONYESHA UTENDAJI KATIKA KUZAA NA KUONGEZEKA


Utangulizi juu ya kuzaa na kuongezeka....................................................................uk. 3

Utangulizi juu ya simulizi.........................................................................................uk. 4

Jua simulizi........ .........................................................................................uk. 5

Fahamu simulizi..........................................................................................uk. 6

Gundua ukweli.............................................................................................uk. 7

Upekee wa tabia ya kuzaa na kuongeze....................................................................uk. 9

Mchakato wa kuzaaa na kuongezek........................................................................uk. 11

Masomo ya vitendo.................................................................................................uk. 12

Kuongoza makundi ya wanafunzi............................................................................uk. 15

Mfululizo wenye umuhimu.......................................................................................uk. 16


## MFULULIZO WENYE UMUHIMU


**Somo la kwanza: JIWE KUU YA PEMBENI............................................................uk. 17**

*"Uhusiano uliorejeshwa"*

**Somo la pili: MSINGI.................................................................................uk. 32**

*"Kaa ndani ya Yesu"*

**Somo la tatu: KUTA...................................................................................uk. 47**

*"Maisha tele"*

**Somo la nne: PAA......................................................................................uk. 62**

*"Ukweli wenye umuhimu"*

# *UTANGULIZI JUU YA*

## KUZAA NA KUONGEZEKA

KUZAA NA KUONGEZEKA (BFAM) ni kozi (mafunzo maalum) na kanuni ya uanafunzi na mtaala ulioundwa kusaidia wafuasi wa Kristo na wale wote wenye hitaji la kuwa wafuasi wa Kristo kufahamu uhusiano wa kimaalumu wanaoweza kuwa nao pamoja na Mungu wa kweli aliye hai. KUZAA NA KUONGEZEKA (BFAM) ni kozi iliyoundwa kuonyesha wafuasi wa Kristo maisha tele wanayoweza kuwa nayo katika uhusiano na Yesu. Watu wameumbwa kuwa na mahusiano wao kwa wao. Iliyo muhimu zaidi watu wameundwa kuwa na mahusiano na Mungu. Madhara ya dhambi yamevunja mahusiano baina ya wao kwa wao na mahusiano baina ya wao na Mungu. Uhusiano wetu uliovunjika umesababisha watu kuishi bila amani wao kwa wao pamoja na uumbaji wote, pamoja na Mungu. Ni kwa sababu hii kwamba katika ulimwengu kuna vita, njaa, vurugu, maradhi, ugonjwa, viongozi dhalimu, na jamii zilizo dharimu. Bila ya kufahamu jinsi gani tunaweza kwenda sambamba na dhambi na jinsi ya kurejesha mahusiano, tutakuwa na hatima ya kuishi maisha ya kukata tamaa.

Habari njema ni kwamba Mungu ametupatia njia ya kutoa hesabu juu ya dhambi na kurejesha mahusiano. KUZAA NA KUONGEZEKA hutafuta kufundisha watu jinsi ya kugundua habari njema inayopatikana katika neno takatifu la Mungu, Biblia. Kama vile watu wanavyogundua habari njema inayopatikana katika simulizi ya Biblia, ukweli wa ki-Biblia uliomuhimu umefunuliwa. Huu ukweli uliomuhimu wa Ki-Biblia unamuwezesha mfuasi wa Kristo kuishi katika mahusiano ya kina na Mungu.

Kanuni ya KUZAA NA KUONGEZEKA kwaajili ya kugundua ukweli wa ki-Biblia huongoza watu kujua jinsi ya kujifunza na kufahamu Biblia. Katika Biblia Mungu hufanya ahadi na wale wanaotafuta kikamilifu kujua ukweli “Ombeni nanyi mtapewa; Tafuteni nanyi mtaona; Bisheni nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; atafutaye huona; naye abishaye hufunguliwa;” (Mathayo7:7-8). Kozi ya KUZAA NA KUONGEZEKA (BFAM) huwafundisha watu jinsi ya kuomba, kutafuta na kubisha. Inawafundisha watu jinsi ya kusoma Biblia na kuangalia ukweli wa Mungu. Ukweli ni huu Mungu ametusamehe dhambi zetu na hutaka kurejesha uhusiano wetu. Kwa wale ambao wanautafuta ukweli wa Mungu kikamilifu na wanaishi katika ukweli unaopatikana  katika Biblia, wameahidiwa kurejeshwa upya kwa Mungu, wanaweza kuishi maisha tele.

Sababu ya kozi hii kuitwa KUZAA NA KUONGEZEKA ni kwamba hatua ya kwanza ya maisha na Mungu ni kugundua kuwa Mungu alituumba tuishi maisha ya kuzaa, tumeitwa maisha ya kuzaaa pande zote mbili kimwili na kiroho (angalia Mwanzo 1:27-28 na Mathayo 28:18-20). Kama vile tunavyowajali watoto wetu wa kimwili hadi kukua pia ni wajibu wetu kama wafuasi wa Kristo kujali kukua kwa watoto wetu wa kiroho. Kwa mfano, mtu peke yake, na makundi ya wanafunzi yanayokua na kukomaa kiroho yatawafanya wengine kuwa wanafunzi kuwaongoza na kuwasahihisha kutokana na ukweli na mamlaka iliyo katika neno la Mungu. Maono ya BFAM na shabaha ya mwisho ni kuendeleza kukua na maisha ya kuzaa kwa sababu maisha ya kuzaa yatasababisha maongezeko ya kiroho.

# *UTANGULIZI JUU YA SIMULIZI*

Kila somo kuhusu kuzaaa na kuongezeka hulenga juu ya simulizi tofauti kutoka katika Biblia. Yesu alisema juu ya simulizi zake na mifano akisema kwamba kila kinachopatikana katika mifano "mambo yaliyofichwa tangu uumbaji wa ulimwengu" (Mathayo 13:34-35) Mungu anasiri zilizofichwa katika simulizi za Biblia na hupanga kwaajili yetu kutafuta na kuzifunua siri hizi.

Masomo ya kuzaa na kuongezeka yakiwa sambamba na kanuni ya kujifunza kuzaa na kuongezeka itakusaidia siri hizi na itakupatia njia ya kuchukua hatua kivitendo, ukweli huu katika maisha yako ya siku kwa siku. Na kama unavyoutumia ukweli unaopatikana katika Biblia utakuongoza katika mahusiano ya kina na Mungu na itazalisha yaliyo upendo, furaha na amani.

Tumepewa mfano ufuatao, katika Biblia, kufafanua jinsi gani ya kutumia kanuni ya kujifunza KUZAA NA KUONGEZEKA kuonyesha umuhimu wa simulizi ya Biblia. Baada ya kusoma utangulizi uliokatika simulizi ya Biblia na simulizi ya Biblia itakayokuongoza kupitia mfululizo wa maswali tisa yatakayokusaidia kuonyesha ukweli wenye nguvu uliojificha katika simulizi. Kabla hujaanza chukua muda kidogo na mwombe Mungu akusaidie kutafuta ukweli uliojificha.

UTANGULIZI KUHUSU SIMULIZI YA BIBLIA: Marafiki waliogundua kuwa Yesu alikuwa na uhusiano wa karibu na Mungu. Mara nyingi walimwona Yesu akichukua muda wa peke yake kuomba Mungu. Pia walikuja kutambua kuwa kwa sababu ya Yesu kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu alikuwa na hekima kuliko mtu yeyote mwingine na alikuwa na nguvu ya kufanya miujiza. Siku moja rafiki zake Yesu walimwomba awafundishe jinsi ya kuomba. Katika kuitikia hitaji lao Yesu aliwapa maneno rahisi ya maombi kuwaonyesha jinsi ya kuomba. Katika hitimisho la maombi Yesu aliwaambia rafiki zake mfano ufuatao:- Akawaambia ni nani kwenu aliye na rafiki, akamwendea usiku wa manane, na kumwambia rafiki yangu amefika kwangu, atoka safarini nami sina kitu cha kuweka mbele yake; na yule wa ndani amjibu akisema, usinitaabishe mlango umekwisha fungwa, nasi tumelala kitandani mimi na watoto wangu; siwezi kuondoka nikupe? Nawaambia ya kwamba, ijapokuwa haondoki ampe kwa kuwa ni rafiki yake, lakini kwa vile asivyoacha kumwomba ataondoka na kumpa kwa kadri ya haja yake. Nami nawaambia ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtaona; bisheni nanyi mtafunguliwa. Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye hufunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi mliowaovu mwajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je baba yenu aliye mbunguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?

Sasa simulizi ambayo umeshaisoma itakupeleka kupitia hatua tatu za mafanikio itakuongoza kwenye ugunduzi wa Kibiblia. Kuna maswali matatu,(3) yakiwa yameunganishwa na kila hatua tatu ambayo inafanya jumla ya maswali 9. Hatua ya kwanza itakusaidia kujua simulizi. Hatua ya pili itakusaidi wewe kufahamu simulizi. Hatua ya tatu itakusaidia kugundua ukweli uliojificha katika simulizi. Unaweza kuchuku muda mrefu, kwa kadri utakavyokuwa na muda mrefu, ndiyo kadri utakavyokuwa na kazi ya maombi ya kutosha kupitia kila hatua.

## HATUA YA 1 – JUA SIMULIZI – OMBA

Kabla hujaweza kugundua siri zinazopatikana katika simulizi ya Biblia au mfano ni lazima kwanza "JUA" simulizi. Kila simulizi ina uthamani wa kawaida na aina tatu. Bali uthamani huu wa aina tatu simulizi haijakamilika. Zifuatazo ni aina tatu muhimu za uthamani katika simulizi.

1. Ni nani wahusika wakuu katika simulizi
2. Ni nini matendo yao wahusika wakuu katika simulizi.
3. Ni nini maelezo kwa mapana na marefu katika simulizi

Kama unaweza kuwatambua wahusika wakuu, matendo yao na maelezo yao katika simulizi halafu utajua (UTAJUA) simulizi. Sasa tutakwenda kutambua wahusika, matendo na maelezo katika simulizi tutasoma. Kwa kutumia peni au penseli (kalamu) chukua muda mfupi kuweka alama kama ifuatavyo:-

- Piga mistari miwili kila mhusika. Mhusika ni mtu. Mara moja unapomtambua mhusika siyo muhimu kupigia mstari mhusika yuleyule kila wakati anapotokea katika simulizi.
- Pigia mstari kila tendo au neno linaloonyesha tendo. Neno linzaloonuyesha tendo ni tendo au tukio.
- Pigia mstari wa zigizaga maelezo maalumu ambayo ni muhimu.

Ufuatao hapo chini ni mfano unaoonyesha jinsi simulizi ya Biblia ambavyo ingeweza kuonekana kama ungeweza kupigia mistari miwili, kupigia mstari na mstari wa zigizaga.
Yesu akawaambia ni nani kwenu aliye na rafiki, akamwendea usiku wa manane na kumwambia, rafiki yangu nikopeshe mikate mitatu kwa sababu rafiki yangu amefika kwangu atoka safarini nami sina kitu cha kuweka mbele yake; na yule wa ndani amjibu akisema, usinitaabishe; mlango umekwishafungwa nasi tumelala kitandani mimi watoto wangu; siwezi kuondoka nikupe;+ nawaambia ya kwamba, ijapokuwa haondoki ampe kwa kuwa ni rafiki yake, lakini kwa vile asivyoacha kumuomba ataondoka na kumpa kadri ya haja yake. + nami nawaambia, ombeni nanyi mtapewa, tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa.+ kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Maana yupi kwenu aliye na Baba ambaye mwanawe akiomba mkate atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa, nyoka? Au akiomba yai, atampa nge? Basi, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Baba aliye mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao wamwombao?

Angalia kama umetofautisha kwa usahihi wahusika katika simulizi. Wafuatao ni waliotofautishwa katika simulizi.

- Yesu
- Wewe
- Rafiki yako wa kwanza anaomba mkate.
- Rafiki yako wa pili juu ya safari
- Yeyote atafutaye na abishaye.
- Baba wa mbinguni
- Roho Mtakatifu

Sasa umeijua simulizi kwa sababu umetofautisha wahusika , matendo yao na maelezo yao juu ya kimaalumu katika simulizi. Chukua dakika chache na angalia kama unaweza kueleza tena kwa sauti au kimya kimya akilini kwako, bila kuangali katika simulizi, utatambua haraka kuwa umekuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu simulizi.

## HATUA YA 2 – FAHAMU SIMULIZI – TAFUTA

**Sasa kwamba UNAJUA simulizi, unakwenda kutafuta KUFAHAMU umuhimu na maana** ya Simulizi, njia iliyobora ya kufahamu maana ya simulizi ni kuangalia mitazamo ya kila mhusika katika simulizi. Katika hatua hii ni muhimu kupiga hatua ndani ya "Viatu" vya kila mhusika kujaribu kuwatofautisha wote.

Jinsi ya kufanya juu ya hili tunauliza maswali mengine matatu.

4. Ni misisimko gani ambayo kila mhusika anaisikia?
5. Ni uchaguzi gani ambao kila mhusika aliufanya?
6. Ni makusudi gani ambayo yapo nyuma ya kila chaguo la mhusika?

Kwa mfano, unapopiga hatua "katika viatu" kwa mhusika wa pili katika simulizi iliyo hapo juu, ambayo ni yako, ni msisimko gani ambao unaweza kujisikia kama unavyokwenda kwenye nyumba ya rafiki yako usiku wa manane kumwomba mkate? Je unakuwa na wasiwasi, je unaogopa? Je ni msisimko gani unaweza kujisikia? Baada ya kuwa umeangalia msisimko inayowezekana ya mhusika halafu fikiri ni uchaguzi gani ambao mhusika ameufanya. Kwa kufikiria mhusika kama ni wewe, ni uchaguzi gani ambao utakuwa umeufanya kama vile ambavyo unakwenda kwa rafiki yako usiku wa manane na kuomba mkate? Je ungeweza kusubiri mpaka asubuhi kuomba mkate? Je ungeweza kumwambia rafiki yako ni nani aliye katika safari ambaye kuna chakula cha kuweka mbele yake? Sisi wote tuna uchaguzi mbalimbalikatika mazingira tunayokutana nayo katika maisha yetu. Inasaidia sana tunapoangalia uchaguzi ambao unapatikata kulinganisha na chaguo lililofanywa katika simulizi.

Kama ulivyoangalia uchaguzi mbalimbali wa mhusika ungetakiwa kutafuta kufahamu makusudi yaliyo nyuma ya chaguo. Tena kwa kufikiria mhusika yuleyule, kama tulikuwa tunaogopa vile ambavyo unaweza kushinda woga wako na kuwa ungegonga mlango wa rafiki yako, nini kusudi lililo nyuma ili uweze kushinda woga wako? Je ni upendo na huruma na rafiki yako?

Je ilikuwa ni wajibu kwa sababu ya mtazamo? Je ni nini kusudi la chaguo lililofanywa? Kwa kuuliza maswali ya msisimko, uchaguzi na makusudi kuchukua KUJUA kwako kwa kiwango cha juu simulizi. 1 itakupa uwezo wa KUFAHAMU umuhimu wa simulizi. Maswali haya mawili yangeweza kuulizwa kwa kila mhusika katika simulizi. Kwa mfano, ni hali gani ya KIMSISIMKO ya rafiki yako ulipobisha mlango usiku wa manane ukitafuta mkate? Je rafiki yako ana chaguo la kukupa mkate au siyo? Halafu angalia makusudi yanayowezekana yaliyo nyuma ya chaguo la rafiki yako kukupa mkate.

Kwa kuchukua hatua ndani ya viatu vya kila mhusika, kwa kuuliza maswali matatu ya msisimko, uchaguzi na makusudi unaweza kutambua kuwa simulizi imekuwa hai. Maranyingi tunapokuwa tunasikia simulizi moja kwa moja tunatazama msisimko, uchaguzi na makusudi ya wahusika bila kuitambua. Maana ya kweli ya simulizi imefunuliwa kupitia maswali haya matatu. Ni kupitia maswali haya mawili kwamba tunaweza kutafuta na KUFAHAMU kweli zilizo katika simulizi.

## HATUA YA 3 – GUNDUA UKWELI – BISHA

Sasa ni kwamba ulishapitia hatua ya 1 na ya 2 KUJUA na KUFAHAMU simulizi, tunakuja katika hatua ya 3 ya KUGUNDUA ukweli uliojificha katika simulizi. Kumbuka, kutokana na mfano huu, Yesu alisema kwamba "UKIOMBA utapokea, kama UKITAFUTA utapata na kama UKIBISHA utafunguliwa." Katika hatua ya 1 TUMEULIZA maswali matatu yaliyotusaidia kujua simulizi katika hatua ya 2 tuliangalia KUTAFUTA kutofautisha na kila mhusika. Na sasa katika hatua ya 3 tunataka kubisha katika mlango wa Mungu na kumtazamia yeye kufungua mlango na kufunua siri zinazopatikana katika simulizi.

Yesu ameshafundisha mafundisho katika maandiko yanaweza kumjulisha pamoja katika amri mbili. Amri ya kwanza ni kumpenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa nafsi, akili na nguvu, na jinsi ya kupenda wengine kama tunavyojipenda wenyewe.

Maswali matatu yanayohusisha maswali mengine matatu ambayo yatasaidia kufunua na siri zinazopatikana katika simulizi ya Biblia. Ni rahisi, kuwa na maswali haya makini.

7. Ni mawazo gani sahihi ya ki-Biblia na matendo yanayopatikana katika simulizi?
8. Simulizi hii inanifundisha kumpenda yeye vizuri zaidi.
9. Simulizi hii inanifundisha nini kuhusu kuwapenda wengine vizuri zaidi?

**SWALI LA UVUMBUZI 1.**

Kama unavyoangalia simulizi ni mawazo gani ya ki-Biblia na matendo yaliyo sahihi? Je ni kweli kwamba Mungu hutuhitaji tumuombe, tumtafute na kubisha? Je haya ni matendo sahihi ya ki-Biblia? Ni nini ulichokipata katika simulizi kinachofundisha kuhusu mawazo sahihi na matendo?

**Chukua dakika chache kuorodhesha:-**

Mara baada ya kutofautisha mawazo na matendo sahihi ya ki-Biblia, swali la pili linauliza, "simulizi hii inanifundisha nini kuhusu tabia ya Mungu itakayonisaidia kumpenda Mungu vizuri zaidi?" kama ulivyoitazama simulizi, je iko sahihi kusema kwamba simulizi inatufundisha kwamba tunaweza kumwangalia Mungu kama Baba aliye mwema? Simulizi hii inatufundisha nini kuhusu Mungu kitakachosaidia kumpenda Mungu kwa moyo wote, nafsi na nguvu?

**SWALI LA UVUMBUZI 3:**
Swali la mwisho linauliza hivi, simulizi hii inanifundisha nini kuhusu kuwapenda wengine vizuri zaidi? Kama ulivyoitazama simulizi, umejifunza nini kuhusu wewe mwenyewe? Na umejifunza nini utawachukuliaje wengine? Yesu alisema tuwapende wengine kwa kiwango kilekile tunavyojipenda sisi wenyewe.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**MUHTASARI** - kama utachukua hatua ya maswali 9 katika kila simulizi katika Biblia itakusaidia KUJUA simulizi, KUFAHAMU simulizi na mwishowe KUGUNDUA siri zilizofichika katika Simulizi. Ufuatao ni muhtasari wa maswali 9 yaliyoorodheshwa.

**JUA SIMULIZI**

1. Wahusika
2. Matendo
3. Maelezo kwa mapana

**FAHAMU SIMULIZI**

4. Msisimko
5. Uchaguzi
6. Makusudi

**GUNDUA UKWELI**

7. Mawazo na matendo sahihi
8. Kumpenda Mungu

Kuwapenda wengine

# *TABIA YA KIPEKEE YA*

# KUZAA NA KUONGEZEKA

Kama ulivyotembalea , kupitia masomo ya KUZAA NA KUONGEZEKA na kanuni ya kujifunza utaona tabia za kipekee katika mtaala ambazo hazipatikani katika aina nyingine za kujifunza Biblia. Zifuatazo ni tabia nne ambazo zitakupatia kufahamu juu ya kutenganisha masomo ya kuzaa na kuongezeka na mafunzo mengine ya Biblia na jinsi ambavyo huleta utoshelevu..

## 1 - KUZAA NA KUONGEZEKA NI MTAALA AMBAO UMELENGA JUU YA SIMULIZI ZA BIBLIA.

Kila somo la kuzaa na kuongezeka limelenga juu ya simulizi ya Biblia. Masomo hayalengi juu ya mafundisho ya maandiko tuu bali simulizi za kweli na mifano inayopatikana katika Biblia. Yesu alipokuja duniani na alipoishi miongoni mwa watu aliowafundisha wafuasi wake kwa kutumia simulizi na mifano. Kwa kweli, kitabu cha Mathayo kimeorodhesha maelezo ya Bwana Yesu kwa nini alitumia mifano. “haya yote Yesu aliwaambia makutano kwa mifano; wala pasipo mfano hakuwaambia neno; ili litimie neno lililonenwa na nabii, akisema, nitafumbua kinywa changu kwa mifano, nitayatamka yaliyositirika tangu awali.”

Katika kifungu hiki Yesu anatupatia ufahamu wa kutosha kuhusu kwanini Mungu amechagua kusema na sisi kwa kutumia simulizi na mifano. Yesu anasema Munguameficha mawazo yake na siri zake katika simulizi na mifano.

Kama utakavyotazama Biblia utaona karibia asilimia 70% ya Biblia imeundwa kwa simulizi, mifano na maelezo ya simulizi uwazi huu Mungu anaouonyesha unaweka umuhimu na nguvu, katika simulizi na mifano. Nia na makusudi ya aliyeunda waumbaji wa KUZAA NA KUONGEZEKA wangehitaji masomo yangelenga juu ya simulizina mifano kwamba mtaala ungemiliki kiwango cha juu cha maandiko katika kila somo la kuzaa na kuongezeka utaona kuna maneno machache ambayo yatatokea moja kwa moja kwenye Biblia. Mtaala vile vile umelenga juu ya simulizi za Biblia kwa sababu ni rahisi zaidi kukumbuka na kusema tena. Kama ulivyogundua siri zilizofichika katika Biblia utakumbuka ugunduzi huu wa kimaalumu kwa kuwa umeutafuta kwa makini na umeupata. Kwa kuongeza, kama unavyoanza kufanya ugunduzi wa ki-Biblia utakuwa na kwako zaidi na yatakuwa ya kusomeka na sahihi kuwashirikisha na wengine.

## 2 - KUZAA NA KUONGEZEKA NI KANUNI ILIYORUHUSIWA

Kama ulivyojifunza kanuni ya kuzaa na kuongezeka umeona kama hukufundusha jinsi ya kuuliza maswali ili wewe mwenyewe kugundua siri za Mungu zilizofichika. Kupitia kanuni hii ya kimaalumu umefundushwa na Roho Mtakatifu jinsi na kutofautisha na kupokea ukweli na ufunuo wa Mungu. Tunakupa changamoto ushiriki ugunduzi wako – habari njema za neno la Mungu – pamoja na wengine. Kanuni ya kuzaa na kuongezeka inakuruhusu wewe kuwa na:-

- Ruksa ya kufikiri wewe mwenyewe
- Ruksa ya kuuliza maswali
- Ruksa ya kufahamu
- Ruksa ya kusikia kutoka kwa Roho Mtakatifu.
- Ruksa ya kushiriki na wengine.

## 3 - KANUNI YA KUZAA NA KUONGEZEKA IMELENGA KATIKA UGUNDUZI

Tunaona katika Biblia yote kwamba Mungu anahitaji watu wanaotafuta na kuupata ukweli. Mungu ameficha siri zake katika neno lake kwamba tungezipata na kuzigundua. Mara nyingi kupitia mchakato wa ugunduzi wa ukweli huu kuna maana kubwa na mguso wa kipekee. Ifuatayo ni mithali rahisi inayoweka wazi uthamani wa uvumbuzi:

- Kama UTANIAMBIA NITASAHAU.
- Kama UTANIONYESHA NITAKUMBUKA
- Kama UTANIHUSISHA NITAFAHAMU.

Siri za kugundua ni mchakato unahitaji nia ya kujihususha. Ni lazima kujihusisha kikamilifu katika kanuni za ya uvumbuzi ili kutafuta ukweli. Njia iliyo bora zaidi ya kugundua siri za Mungu ni kupitia kuhusisha kundi. Ingawa unaweza kujifunza simulizi na kugundua ukweli kwa mahusiano yako na Mungu, waweza kujifunza vilevile simulizi na kundi dogo na kujifunza uvumbuzi zaidi kutoka kila mmoja kwa mwingine.

## 4 - KUZAA NA KUONGEZEKA NI KANUNI ILIYOJENGWA KATIKA UTII

Kuna mguso mdogo sana wa kibinafsi katika kukata utepe wa siri za Mungu katika maandiko kama hatutafunga na kuchukua hatua za ukweli katika maisha yetu. Kifuatacho ni kifungu cha maandiko ambacho hutuambia kwamba tutapokea baraka kwa Mungu kama tutatumia kanuni yake na ukweli katika maisha yetu. “lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu kwa sababu mtu akiwa msikiaji wa neno tu wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyetazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali utendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake” (Yakobo 1:22-25)

Mchakato wa kuzaa na kuongezeka hauangalii mchakato wa ugunduzi peke yake namna ya mchakato wa kimaombi wa ugunduzi wa kibinafsi. Pindi tunapogundua ukweli wa Mungu ni lazima kutafuta kufahamu ni jinsi gani tunauishi huo ukweli.
Mfikirie 2 TIMOTHEO ambavyo husema katika maandiko; “kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki; Ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.+” (2 Timotheo 3:16-17)

Angalia kifungu hiki cha maandiko kinavyosema kwamba maandiko yote “YAFAA KWA” hii inashauri kuwa kama ukweli wa maandiko utatumiwa halafu nafaa kwa mafundisho, kwa kuonya (kukemea) kusahihisha na kufunza. Kifungu hiki ijapokuwa hakitupi ahadi ya moja kwa moja kwamba maandiko yatatufundisha moja kwa moja, kutuonya, kutusahihisha kutufunza. Ni lazima tuwe na kusudi lenye nia kuhusu andiko lifuatalo kufundisha, kuonya, na kutufunza. Katika mchakato wa ugunduzi wa KUZAA NA KUONGEZEKA kwanza ni lazima tutambulishe ukweli wa maandiko unaofundishwa. Baada ya kutambulisha ukweli huu turuhuisu maandiko yatukemee, yartusahihishe na kutufunza. Ufuatao ni mfulululizo wa maswali tunauliza kuruhusu maandiko kutukemea, kutusahihisha na kutufunza.


KUKEMEA: Inahusika na wakati uliopita ni jinsi gani nafanya mawazo na matendo yangu binafsi kuhusu Mungu kulinganisha na mawazo na matendo sahihi ya ki-Biblia nililojifunza katika simulizi?

KUSAHIHISHA: inahusika na wakati, wako uliopo.

Nifanye nini kusahihisha mawazo na matendo yangu mabaya?

KUFUNZA: inahusika na wakati wako ujao.
nitaitikiaje wakati ujao nitakapokutana na hali ya changamoto ya mawazo na matendo sahihi ya ki-Biblia.

# Mchakato wa kuzaaa na kuongezeka unavyofafanuliwa




**HATU TANO KILA SOMO**

Kila somo linachukua hatua tano na kila hatua inachukua  muda sawasawa na mahali sahihi pa kuvuna tunda.

## KIINI CHA SOMO – ANDAA UDONGO

kiini cha somo kimeundwa kuandaa udongo wa akili yako na moyo wako kama unavyoanza mchakato wa kutafuta ukweli uliopewa na Mungu katika Biblia.

## SIMULIZI YA BIBLIA – PANDA MBEGU

Simulizi ya Biblia ni mbegu iliyopandwa katika nafsi ambayo itaanza kuota, kuchipua kutoa majani, na kuota katika maarifa na kweli. Kabla ya kusoma simulizi hakikisha unachukua muda wa maombi, kumuomba Mungu afungue ufahamu wako na moyo wako katika ukweli wa Biblia.

## MCHAKATO WA UGUNDUZI – MAJI NA RUTUBISHA

Tumia maswali 9 kumwagilia na kurutubisha mbegu, neno la Mungu, ili kusaidia kugundua ukweli unaopatikana katika simulizi. Jiweke wewe mwenyewe ndani ya “VIATU” wahusika.

1. Je wahusika katika simulizi ni akina nani?
2. Ni matendo gani ya wahusika katika simulizi?
3. Ni maelezo gani yapo katika simulizi?
4. Ni misisimko gani ambayo kila mhusika anahisi?
5. Ni uchaguzi gani ambao kila mhusika anao?
6. Ni kusudi gani ambalo liko nyuma ya uchaguzi wa kila mhusika?
7. Ni mawazo na matendo gani ya ki-Biblia yaliyo sahihi yanayopatikana katika simulizi?
8. Simulizi inafundisha nini kuhusu tabia ya Mungu itakayonisaidia kumpenda Mungu vizuri zaidi?
9. Simulizi hii inanifundisha nini kuhusu kuwapenda wengine vizuri zaidi.

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA – KUPUNGUZA

Maandiko ya kusoma ya nyongeza yamejumrishwa kusaidia kuzuia mafundisho ya uongo ambayo yanaweza kuundwa nje ya simulizi peke yake. Soma kupitia maandiko haya kusaidia kujibu maswali ambayo unaweza kuwa nayo katika simulizi ya Biblia

## MAOMBI NA MASWALI/ HITIMISHO – KUVUNA MATUNDA

Maombi na maswali na hitimisho yanasaidia mchakato wa kuvuna ukweli unaopatikana katika kila simulizi na kuutumia ukweli huu katika maisha yetu binafsi. Ikiwa imelenga katika mawazo na matendo sahihi ya ki-Biblia yanayopatikana wakati wa mchakato wa ugunduzi, itikia maswali yafuatayo:-

- KUKEMEA: inahusika na wakati wako uliopita. Ni kwa jinsi gani mawazo na matendo yangu binafsi kuhusu Mungu kulinganisha na mawazo na matendo sahihi ya ki-Biblia niliyojifunza kutoka katika simulizi.
- KUSAHIHISHA :- inahusika na wakati wako uliopo. Nitafanyaje ili kusahihisha mawazo na matendo yangu mabaya?
- KUFUNZA :-inahusika na wakati wako ujao. Ni jinsi gani nitaitikia wakati ujao nitakapokutana na hali itakayoleta changamoto juu ya mawazo na matendo sahihi ya kiBiblia?

# TUMEPEWA KARAMA

SOMO
P-1

## Watu Watatoa Hesabu Ni Jinsi Gani Wametumia Karama Zao

### KIINI CHA SOMO – ANDAA UDONGO

Biblia inasema watu watakwenda kutoa hesabu kwa Mungu kwakile walichokifanya kwa ajili ya karama waliopewa na Mungu.

ANDIKO LA UFUNGUZI: basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu. (WARUMI 14:12)

### SIMULIZI YA BIBLIA – PANDA MBEGU

Utangulizi unatoa habari ili kufahamu simulizi.

Yesu alisema na wanfunzi wake kupitia mifano. Mfano ni simulizi ambayo inaweza kutumiwa kuonyesha kanuni.

Simulizi Ya Biblia Inaanza Hapa.

“Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake, akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja taranta tano, na mmoja taranta mbili, na mmoja taranta moja: kila mtu kadri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea taranta tano akaenda akafanya biashara nazo, akachuma faida taranta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye akachuma nyingine mbili tena faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukia chini, akaificha fedha ya Bwana wake. Baada ya siku nyingi akaja Bwana wa watumwa wale, akafanya hesabu nao. Akaja yule aliyepokea taranta tano, akaleta taranta nyingine tano, akasema, Bwana, uliweka kwangu taranta tano; tazama, taranta nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, vema, mtumwa, vema,mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya wengi; ingia katika furaha ya Bwana wako. akaja na yule aliyepokea taranta mbili, akasema, Bwana, uliweka kwangu taranta mbili; tazama talantanyingine mbili nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya wengi; ingia katika furaha ya Bwana wako. Akaja na yule aliyepokea taranta moja, akasema wana, nilitambua kwamba wewe ni mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya, basi nikaogopa, nikaificha taranta yako katika ardhi; tazama, unayo iliyo yako. Bwana wake akajibu, akamwambia, wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi, ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoa riba; nami nikija ningaliipata iliyo yangu na faida yake. Basi mnyang’anyeni taranta hiyo, mpeni yule aliye nazo taranta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alichonacho atanyang’anywa. Na mtumwa yule asiyefaa, mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno”.
(MATHAYO 25:14-30)

### MCHAKATO WA UGUNDUZI – MAJI NA KURUTUBISHA

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA – KUPUNGUZA (Pogoa)

(WARUMI 12:3-8; 1 WAKORINTHO 10:31; 2 WAKORINTHO 5:10; WAEFESO 4; WAFILIPI 4:14 – 19; UFUNUO 20:11-15)

### MAOMBI NA MASWALI / MSINGI – KUVUNA MATUNDA

### HITIMISHO –

Biblia inasema kuwa watu watatoa hesabu kwa Mungu ni kwa jinsi gani wanaishi maisha yao. Maisha ni zawadi kutoka kwa Mungu. Mungu hutaka maisha yetu yazae matunda.

# KUMPENDA MUNGU

SOMO P-2

Amri Iliyomuhimu Zaida

## KIINI CHA SOMO – ANDAA UDONGO

Yesu aliamuru wafuasi wake kufanya mambo mengi. Yesu hutaka watu wote wamfuate na wafanye kile ambacho husema. Jambo la muhimu zaidi ambalo wafuasi wa Kristo wanalotakiwa kufanya ni kumpenda Mungu na kusikiliza maneno yake.

NENO LA UFUNGUZI: Na mmojawapo wa Waandishi akafika, akawasiki wakisemezana naye, akatambua yakuwa amewajibu vema, akamwuliza katika amri zake ni ipi iliyo ya kwanza? Yesu akamjibu, ya kwanza ndiyo hii, sikia, Israel, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. Na ya pili ndiyo hii, mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. (MARKO 12:28-31).

## SIMULIZI YA BIBLIA – PANDA MBEGU

Utangulizi unatoa habari ili kufahamu simulizi.

Yesu alukuwa na wanafunzi wake.

Simulizi Ya Biblia Inaanza Hapa.

“ikawa katika kuenenda kwao aliingia katika kijiji kimoja; mwanamke mmoja jina lake Martha akamkaribisha nyumbani kwake.+ naye alikuwa na umbu lake aiitwae Mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake. Lakini martha alikuwa akihangaika kwa utumishi mwingi; akamwendea akisema, Bwana, huoni vibaya hivyo ndugu yangu alivyoniacha nitumike peke yangu? Basi mwambie anisaidie. Bwana akajibu akamwambia, Martha, Martha, unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; lakini. Kinatakiwa kitu kimoja tu; na mariamu amelichagua fungu lililojema ambalo halitaondolewa. (LUKA

## MCHAKATO WA UGUNDUZI – MAJI NA KURUTUBISHA

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA – KUPUNGUZA (Pogoa)

(MATHAYO 22:36-37; LUKA 11:42; JAKOBO 1:12; 1 YOHANA 2:4 – 5; 1 YOHANA 4)

## MAOMBI NA MASWALI / MSINGI – KUVUNA MATUNDA

## HITIMISHO –

Amri iliyomuhimu zaidi iliyotolewa na Bwana Yesu ni watu wampende yeye na wamsikilize anachosema.

# KUPANDA KWA UMINIFU NENO LA MUNGU

SOMO
P-3

Maisha Yanayozaa Matunda Tele

## KIINI CHA SOMO – ANDAA UDONGO

Biblia ni neno la Mungu. Wafuasi wote wa Kristo wameitwa kusikia na kujua maneno hayo. Biblia hufunza watu wote kusikia maneno ya Munguna kuyaishi. Shetani hapendi watu wajue na kufahamu maneno ya Mungu. Shetani hupenda kuyachukua maneno ya Mungu kutoka kwenye mioyo yetu. Tunapoyasikia maneno ya Mungu na kuyaishi maisha yetu yatakuwa na matunda.

ANDIKO LA UFUNGUZI: Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu – ZABURI 119:105

## SIMULIZI YA BIBLIA – PANDA MBEGU

Utangulizi unatoa habari ili kufahamu simulizi.

Yesu anazungumza na kundi kubwa la watu. Kundi hili la watu ni kutoka sehemu mbalimbali.

Simulizi Ya Biblia Inaanza Hapa.

“Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake; naye alipokuwa akizipanda, nyingine zilianguka karibu na njia, zikakanyagwa ndege wa angani wakazila. Nyingine zikaanguka penye mwamba; zilipoanza kumea zikakauka kwa kukosa rutuba. Nyingine zikaanguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja nazo ikazisonga. Nyingine zikaanguka penye udongo mzuri; zikamea, zikazaa moja kwa mia. Alipokuwa akinena hayo alipaza sauti akisema, mwenye masikio yakuyasikia na asikie. Na huo mfano maana yake ni hii; mbegu ni neno la Mungu. Wale wa karibu na njia ndio wasikiao, kisha huja ibilisi akaliondoa hilo neno mioyoni mwao, wasije wakaamini na kuokoka. Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi, huamini kitambo kidogo, na wakati wa kujaribiwa hujitenga. Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lolote. Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu wa wema wa mioyo hulisikia neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa kuvumilia.”(LUKA 8:5-8,11-15)

## MCHAKATO WA UGUNDUZI – MAJI NA KURUTUBISHA

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA – KUPUNGUZA (Pogoa)

(ZABURI 119; YOHANA 10:27; YOHANA 15:16; WAFILIPI 1:9-11; WAKOLOSAI 1:9-12; 1PETRO 5:8)

## MAOMBI NA MASWALI / MSINGI – KUVUNA MATUNDA

## HITIMISHO –

Watu wa Mungu wanaposikia maneno ya Mungu na kuishi sawa na maneno haya, maisha yao yanazaa matunda mazuri. Ni muhimu kwamba wafuasi wa Kristo wasimruhusu shetani au kujali ulimwengu kuchukua maneno ya Mungu miongoni mwao.

# *KUUNGANISHA MAKUNDI YA MADARASA*

## SIFA NA KUBUDU

- Mwalike Mungu awe katikati ya mkutano kupitia maombi na kundi la kuabudu.
- Toa muda wa shukrani na ushuhuda mbele za watu.

## GUNDUA SOMO NA KULIFANYIA KAZI

HATUA YA 1 – KIINI CHA SOMO
Shiriki kiini cha somo na andiko la ufunguzi pamoja na kundi.

HATUA YA 2 – SIMULIZI YA BIBLIA
Shiriki utangulizi na simulizi pamoja na kundi.

HATUA YA 3 – MCHAKATO WA UGUNDUZI
- Jua simulizi
- Fahamu simulizi
- Gundua ukweli wa ki-Biblia

HATUA YA 4 - MAANDIKO YA NYONGEZA YA KUJIFUNZA
Angalia mawazo sahihi ya ki-Biblia na matendo yaliyogunduliwa na kundi kuthibitisha kama ni ugunduzi wa kweli wa ki-Biblia.

HATUA YA 5 – MASWALI NA MAJIBU NA HITIMISHO
Inahusika zaidi na ugunduzi uliopatikana kwenye simulizi, itikia maswali yafuatayo:- (kufundisha)

KEMEA – inahusika na wakati wako uliopita
ni jinsi gani ninafanya mawazo na matendo yangu binafsi kuhusu Mungu kulinganisha na mawazo ya ki-Biblia na matendo niliyojifunza katika simulizi?

SAHIHISHA – inahusika na wakati wako uliopo.
Inahusika kusahihisha mawazo na matendo yangu mabaya?

## KUISHI KATIKA JAMII

KUKUA KATIKA KRISTO
Ulizia kundi, ni jinsi gani walitendea kazi ukweli waliojifunza katika mkutano wa wanafunzi uliopita?

KUSHIRIKI UKWELI PAMOJA NA WENGINE.
Ulizia kundi ni jinsi gani wameshiri simulizi ya Biblia na wengine?

Ulizia kundi, ni nani unayekwenda kushiriki pamoja naye simulizi hii kati ya sasa na mkutano wa wanafunzi ujao?
KUWAJALI WENGINE
Ulizia kundi, ni jinsi gani wamekwenda kuitikia katika kundi letu na mahitaji ja jamii kutoka katika kundi letu na mahitaji ya jamii kutoka katika mkutano wa uanafunzi uliopita?

Ulizia kundi, je kuna wajibu wowote au tatizo la kuwa nalo makini ambalo lipo kati ya kundi letu au jamii?

Ulizia kundi, ni jinsi gani kundi limeitikia wajibu mpya na matatizo?

# *Mfululizo Uliomuhimu Zaidi*

## KUJENGA NYUMBA AMBAYO MUNGU ATAISHI NDANI YAKE

Masomo ya kwanza 52 ya KUZAA NA KUONGEZEKA yanaitwa mfululizo uliomuhimu zaidi. Mfululizo huu ni wa kujifunza mwaka mmoja umeundwa na seti ya masomo manne ambayo kila seli lina masomo 13. Mfululizo uliomuhimu zaidi umetengenezwa baada ya mpangilio wa ujenzi wa nyumba. Kila seti hizo za masomo manne zinaitwa baada ya sehemu mbalimbali za ujenzi wa nyumba . sehemu hizo nne za ujenzi wa nyumba ni JIWE LA PEMBENI, MSINGI, KUTA, PAA.
Ufuatao ni ufafanuzi juu ya hizo seti za masomo manne.



SOMO LA JIWE KUU LA PEMBENI – UHUSIANO ULIOREJESHWA.
Somo la seti ya jiwe kuu la pembeni inalenga juu ya somo linalohusu jinsi Mungu alivyoumba vitu vyote. Ukweli huu unaimarisha ulimwengu kuwa na mtazamo uliosahihi wa ki-Biblia. Somo la pili limeimarishwa kuwa watu waliumbwa tofauti kuliko viumbe wengine waliosalia katika uumbaji. Tumeumbwa kwa mahusiano ya kimaalumu na Mungu. Somo la tatu na la nne linahusu jinsi mwanadamu alivyodanganywa na nyoka (shetani). Mtu wa kwanza alimwasi Mungu na matokeo yake uhusiano wetu na Mungu ulivunjika. Masomo yaliyobaki yanaonyesha mpango mkubwa wa kukomboa na kupatanisha watu kuelekea katika kuwa na uhusiano na yeye.




SOMO LA SETI YA MSINGI – KUKAA NDANI YA YESU.
Somo hili limelenga umuhimu wa kutii amri za Yesu Kristo. Yesu alisema “basi kila asikiaye haya maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba” (MATHAYO 7:24). Somo la seti ya msingi huonyesha jinsi ya kuimarisha msingi wa ki-Biblia ulioimara uliojengwa katika maisha ya utii.



SOMO LA SETI YA KUTA – MAISHA TELE.
Kuta za nyumba ndio zinazoangaliwa na watu kwa nje ya nyumba. Ukweli huu ni sawa na wafuasi wa Kristo. Wafuasi wa Kristo lazima waonekane na kutenda katika njia inayomwonyesha Mungu kwa wale wanaomzunguka seti ya somo hili inalenga makusudi muhimu ya familia ya Mungu duniani.



SOMO LA SETI YA PAA – UKWELI ULIO MUHIMU ZAIDI.
Somo la seti hii ya mwisho linajumulisha ukweli wa msingi wa imani ya Mkristo. Paa imetengenezwa kuzuia vitu vya nje au vitu visivyotakiwa.
Somo la seti la paa limeundwa kuzuia mafundisho potofu (mafundisho ya uongo) kwa kuonyesha msingi wa kweli wa kibiblia wa imani ya Mkristo.




JIWE KUU LA PEMBENI | MSINGI | KUTA | PAA

“Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu. Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni. Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho.” (WAEFESO 2:19-22).

KUZAA NA KUONGEZEKA

www.iBFAM.org



# UHUSIANO ULIOREJESHWA

Mpangilio wa Masomo! **1** *Jiwe la Pembeni*

"*Kwa kuwa katika yeye ulipendeza utimilifu wote ukae na kuwa yeye huvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake kwa yeye ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni*" (Kolosai. 1:19-20)

# *Jiwe la Pembeni*

Mpangilio wa pili wa somo: *Ukurasa*

---

**MASOMO:**


1-1 MUNGU, MUUMBA WA MBINGU NA NCHI........................................ukurasa 19
aliumba kila kitu

1-2 Uumbaji mahsusi wa Wanadamu.........................................................ukurasa 20
alimuumba kwa ajili ya uhusiano mahsusi na Yeye na pia baina yao

1-3 Shetani ni Mlaghai.........................................................................ukurasa 21
alikuja, kuiba, kuua na kuharibu

1-4 Adamu na Eva Walimuasi Mungu.............................................................ukurasa 22
sasa tunaishi katika laana

1-5 Uzao Mteule. ...................................................................................ukurasa 23
uhusiano mahsusi wa Mungu na Abrahamu

1-6 Mungu anamjaribu Abrahamu................................................................ukurasa 24
Abraham anamtii Mungu

1-7 Kuna uzima baada ya kifo.................................................................. ukurasa 25
uzima baada ya kifo utakuwa kwenda mbinguni au Jehanum

1-8 Yesu Kristo......................................................................................ukurasa 26
Mungu kamili na mwanadamu kamili

1-9 Mpango wa Mungu wa Upatanisho kwa Wanadamu.............................ukurasa 27
Kuchukua adhabu kwaajili ya Dhambi na kurudisha uhusiano

1-10 Yesu Anashinda Mauti........................................................................ukurasa 28
Kufufuka kwake kunadhihirisha alikuwa nani

1-11 Nifanye nini nipate kuokoka?...............................................................ukurasa 29
amini

1-12 Tunaitikiaje upendo wa Mungu............................................................ukurasa 30
toba

1-13 Mimi ni rafiki wa Bwana Yesu.............................................................ukurasa 31
Ninabaki katika upendo wake kwa kutii amri zake

# MUNGU MUUMBA WA MBINGU NA NCHI

SOMO 1-1

*Aliumba Kila Kitu*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Kuna Mungu mmoja tu. Anajua yote, ana nguvu zote, yupo kila mahali na aliumba vitu vyote. Kutoka utupu. Amri ya Mungu ilifanya ulimwengu wote. Mungu aliumba vitu vyote kwa ukamilifu, kwa kuwa Mungu nimkamilifu sana.

Andiko la msingi *: Ameiumba dunia kwa uweza wake, ameuthibitisha ulimwengu kwa heshima yake, na kwa ufahamu wake amezitandika mbingu.(Jeremiah 51:15)*

## Simulizi Ya Biblia -*Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Mungu alikuwako kabla ya vitu vyote. Biblia inasema kuwa Mungu aliumba dunia na vitu vyote vilivyomo duniani kwa siku sita. Katika siku tano za kwanza Mungu aliumba nuru, jua na mwezi, nyota na anga, maji na nchi. Aliumba pia miti na majani na kila aina ya kiumbe, cha baharini na kila aina ya ndege wa angani wenye uwezo wa kuzaana. Mungu akaona ya kuwa ni vyema. Habari yetu inaanzia siku ya sita.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

Mungu akasema, "***nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake, wanyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu, kwa jinsi zake; ikawa hivyo. Mungu akafanya mnyama wa mwitu kwa jinsi zake, na mnyama wa kufugwa kwa jinsi zake, na kila kitu hai kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi zake; Mungu akaona ya kuwa ni vema. Mungu akasema, na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia. Na kila chenye kutambaa kitambae juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake. Kwa mfano wa Mungu, alimuumba mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia Mungu akawaambia, zaeni mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi*"** *(Zaburi. 1:24-28)*

## **MCHAKATO wa UGUNDUZI** - Maji na rutubisha

## **MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA** - Kupunguza

*(WaKolosai. 1:16; Ufunuo:4:11; Zaburi.33:6 - 9; Isaya. 40:21 - 28; Waebrania. 11:3)*

## **MAOMBI NA MASWALI/MSINGI** -Kuvuna Matunda *(2 Timotheo 3:16-17)*

## ===HITIMISHO

Ulimwengu na vyote vilivyomo havikuwepo kwa ajali, kuna muumba mmoja, na ni Mungu. Kila alichoumba Mungu ni kikamilifu.

# UUMBAJI MAHSUSI WA WANADAMU

SOMO 1-2

## Aliumba Kwaajili ya Uhusiano Mahsusi na Mungu na pia baina yao

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Mungu alimuumba mtu awe tofauti na wanyama. Wanadamu waliumbwa kuonyesha asili ya Mungu. Mungu alimuumba mtu kuwa na uhusiano mahsusi na yeye. Mungu alimuumba mtu pia kuwa msaidizi.

Andiko la msingi: Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo yako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana (zaburi 139:14)

### Simulizi Ya Biblia - Kupanda Mbegu

Biblia inatueleza kuwa Mungu aliumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo, na Mungu akaona kuwa vyote ni "vyema"

Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. Bwana Mungu akasema si vema mtu huyo awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje, kila kiumbe hai, jina alilokiita adamu likawa ndilo jina lake. Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni, lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu, aliyefanana naye. Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito, naye akalala, kasha akatwaa ubavu wake mmoja; akafunika nyama mahali pake, na ule ubavu alioutwaa katika Adamu, Bwana Mungu akamfanya mwanamke, kwa Adamu. (Mwanzo 2:7, 18-22)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Zaburi 24:1; zaburi 100:3; zaburi 139:13-16; waefeso 5:28, 31; Warumi 8:38-39)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO - Mungu aliwaumba mwanamume na mwanamke mahsusi. Wako sawa. Waliumbwa waishi kwa ushirikiano wao kwa wao. Waliumbwa pia waishi kwa ushirikiano na Mungu.

# SHETANI MLAGHAI

## Alikuja Kuiba, Kua, na Kuharibu

SOMO 1-3

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Uovu upo. Shetani ni mwovu. Shetani anamchukia Mungu. Shetani anauchukia uumbaji mkamilifu wa Mungu. Kwa sababu Shetani anauchukia uumbaji mkamilifu wa Mungu, alikuja duniani akijifanya nyoka ili kuuharibu uhusiano maalumu kati ya Mungu na mwanadamu.

Andiko la msingi: Mwivi haji ila aibe, na kuchinja, na kuharibu, mimi nalikuja, ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele. (Yohana 10:10)

### Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Mungu aliwaweka mwanamume na mwanamke na kuwaweka katika bustani nzuri. Mungu akamwambia mwanadamu kula matunda kutoka katika miti yote ya bustani isipokuwa mti mmoja, Mungu akasema, "matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

Basi nyoka alikuwa mwelevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi hivi ndivyo alivyosema Mungu, msile matunda ya miti yote ya bustani? Mwanamke akamwambia nyoka, matunda ya miti ya bustani twaweza kula; lakini matunda ya mti uliokati kati ya bustani Mungu amesema, msiyale, wala msiyaguse msije mkafa. Nyoka akasema hakika hamtakufa, kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakapokula matunda ya mti huo , mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu mkjua mema na mabaya. Bwana Mungu akamwambia mwanamke nini hili ulilofanya? Mwanamke akasema, nyoka alinidanganya nikala. Bwana Mungu akamwambia nyoka kwa sababu umefanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani walioko mwituni, kwa tumbo utakwenda na mavumbi utakula siku zote za maisha yako; name nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa na wewe utamponda kisigino" (Zaburi3:1-6, 13-15).

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Marko1:9-13; 2 Thesalonike 2:8-10; ufunuo 12:9; 1 Petro 5:8)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO - Tamaa mbaya za Shetani, zilimfanya kumpinga Mungu na mipango yake. Mipango ya Shetani duniani ilianza kwa kumshawishi Eva. Shetani alimdanganya eva kumwasi Mungu. Shetani anamchukia mwanadamu na uhusiano wake maalumu na Mungu.

# ADAM NA EVA WALIMUASI MUNGU

SOMO 1-4

## Sasa tunaishi katika laana

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Shetani alikuja na kumdanganya Eva kumwasi Mungu. Kumwasi Mungu ni dhambi. Mungu anaadhibu dhambi. Matokeo ya dhambi kwa Adamu na Eva ni kuwa uhusiano wao na Mungu ulivunjwa. Matokeo ya dhambi ni shida adha na kifo.

Andiko la msingi: Kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti, na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi. (Romans 5:12)

### Simulizi Ya Biblia - Kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Wanadamu wa kwanza kuumbwa na Mungu waliitwa Adamu na Eva. Mti katika habari hii ni mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Mungu alisema, wangalikula matunda ya miti yote isipokuwa mti huu.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kuwa chakula, wapendeza macho nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala, wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo, kasha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, alitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na Mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu akawaona. Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia uko wapi? Akamwambia nalisikia sauti yako bustanini nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi, nikajificha, akasema, ni nani aliyekwambia yakuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? Adamu akasema, huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja name ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. Bwana Mungu akamwambia mwanamke, nini hihi ulilolifanya? Akamwambia mwanamke, hakika nitakuzidishia uchungu wako na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto na tamaa yako itakuwa kwa mumeo naye atakutawala. Akamwambia Adamu, kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nilikuagiza, nikisema usiyale, ardhi imelaaniwa kwaajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; michongoma na miiba itakuzalia nawe utakula mboga za bondeni kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, na mavumbini utarudi" (Mwanzo 3:6-13, 16-19)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Yakobo 1:13-15; Isaya 59:2; Warumi3:23; Warumi 6:23; 1 Yohana 3:5)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timothy 3:16-17)

===HITIMISHO - Mashaka na kutokumtii Mungu kulivunja uhusiano na Mungu. aliyemkamilifu hawezi kuivumilia dhambi. Wanadamu wote wamefanya dhambi, Matokeo ya dhambi ni shida, adha na kifo.

# UZAO MTEULE

SOMO 1-5

## Uhusiano Mahsusi wa Mungu na Abraham

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Matokeo ya dhambi ya Adamu na Eva yalirithiwa na wanadamu wote. Mungu aliufanya mpango wa kuurudisha uhusiano na mwanadamu. Mungu aliweka ahadi kwa mtu aliyeitwa Abrahamu. Mungu alimuahidi abrahamu kuwa kupitia uzao wake, wanadamu watapatanishwa na Mungu.

Andiko la msingi: Bwana akamwambia Abramu, toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako, uende mpaka nchi nitakayo kuonyesha; nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka, nami nitawabariki wakubarikio naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa" (Zaburi 12:1-3)

### Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Abrahamu alikuwa ni mtu aliyemtii Mungu aliposema naye. Mungu aliichagua familia ya Abrahamu kuwa ndiyo familia itakayomshinda Shetani, na mataifa yote yatabarikiwa. Abrahamu hakuamini kuwa Mungu angempa mwana kupitia mke wake, hivyo Abrahamu alifanya mambo kwa njaa yake na siyo kwa mpango wa Mungu. Abrahamu na mke wake hawakuwa na mtoto hivyo Abrahamu akazaa mtoto na mjakazi wake. Mtoto huyu aliitwa Ishmael.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-
Abrahamu alipokuwa mtu wa miaka tisini na kenda, Bwana akamtokea Abrahamu akamwambia, mimi ni Mungu mwenyezi, uende mbele yangu ukawe mkamilifu. Nami nitafanya agano kati yangu na wewe name nitakuzidisha sana. Abrahamu akaanguka kifulifuli. Mungu akamwambia, akasema, mimi agano langu nimefanya nawe. Nawe utakuwa baba wa mataifa mengi, wala jina lako hutaitwa tena Abramu, lakini jina lako litakuwa Ibrahimu, kwani nimekuweka uwe baba wa mataifa mengi. Nitakufanya uwe na uzao mwingi sana, name nitakufanya kuwa mataifa, na wafalme watatoka kwako. Agano langu nitalifanya imara kati ya mimi na wewe, na uzao wako baada yako, na vizazi, vyao kuwa agano la milele, kwamba nitakuwa Mungu kwako na kwa uzao wako baada yako. Ndipo Ibrahimu akaanguka kifulifuli akacheka, akasema moyoni; je! Mtu wa umri miaka mia, kwake atazaliwa mtoto? Naye Sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa? Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako. Mungu akasema, sivyo lakini Sala mkeo atakuzalia mwana wa kiume, nawe utamwita jina lake Isaka. Nami intafanya agano langu imara kwake, kuwa agano la milele, kwaajili ya uzao wake baada yake. (Mwanzo 17:1-7, 15-19)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Mwanzo15:1-6; Waebrania 11:8-12; Wagalatia 3:16-18; Isaya 51:1-2; Yakobo2:23)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO - Mpango wa Mungu wa kumpatanisha mwanadamu na yeye, ulianza na Ibrahimu Mungu aliahidi kuwa kupitia uzao wa Ibrahimu, ulimwengu wote ungelibarikiwa. Mungu aliahidi kuwa kupitia uzao wa Ibrahimu watenda dhambi wote wangelikombolewa.

# MUNGU ANAMJARIBU ABRAHAM

SOMO 1-6

## Abraham Anamtii Mungu

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Ahadi zote ambazo Mungu alizifanya na Abrahamu zilitegemea na uhai wa Isaka. Abrahamu alijaribiwa na Mungu. Abrahamu alitii amri za Mungu. Abrahamu aliamini kuwa Mungu hawezi kusema uongo.

Andiko la msingi: Kwa imani Abrahamu alipojaribiwa,akamtoa Isaka awe dhabihu nayeye aliyezipokea hhizo ahadi alikuwa akimtoa mwanawe, mzaliwa pekee nay eye aliyeambiwa, katika Isaka uzao wako utaitwa, alihesabu ya kuwa Mungu anaweza kumfufua hata kutoka kuzimu; akampata tena toka huko. Kwa mfano. (Waebrania 11:17-19)

### Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi*.

Hapo zamani Mungu aliruhusu sadaka ya damu kufunika dhambi. Kutoa sadaka lililkuwa tendo la kidini la kujitakasa. Lilikuwa pia tendo la kuabudu.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

Akasema, umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketeza huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. Ibrahimu akaondoka alfajiri akatandika punda wake akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwaajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Mungu. Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake, akapaona mahali pakali mbali. Ibrahimu akawaambia vijana wake, kaeni ninyi hapa pamoja na punda na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu na kuwarudia tena. Basi Ibrahimu akazitwaa kuni na hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe akatwaa moto na kisu mkononi mwake wakaenda wote wawilipamoja. Isaka akasema na Ibrahimu Babake akinena, Babangu! Naye akasema mimi hapa, mwanangu. Akasema tazama! Moto upo, na kuni, yupo wapi mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa? Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwanakondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kasha akamfunga Isaka mwanawe akamuweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni. Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe, ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguniakasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema mimi hapa. Akasema usimnyoshee kijana mkono wako wala usimtende neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee. Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. (Mwanzo 22:2-13)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Warumi 4:1-24; Yakobo 2:21-22; Mwanzo 22:15-18)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO Kutolewa sadaka kwa Isaka na Abrahamu kulionyesha imani ya Abrahamu kwa Mungu. Abrahamu alimtii Mungu. Abrahamu alipojaribiwa na Mungu alimwamini na kumtii Mungu. Miaka mingi baada ya habari hii ya ibrahimu Mungu aliitoa sadaka ya maramoja ambayo ilifidia dhambi zote za wanadamu

# KUNA UZIMA BAADA YA KIFO

SOMO 1-7

## Uzima baada ya kifo, utakuwa Kwenda Mbinguni au jahanum

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Maandiko yanatufundisha sisi kuhusu maisha baada ya kifo. Baada ya kifo, watu watakwenda mbinguni au kuzimu (jehanamu). Mbinguni ni mahali ambapo Mungu yuko. Mbinguni kuna furaha tele kwa sababu ya uwepo wa Mungu huko mbinguni. Kuzimu (Jehanamu) ni mahali pa mateso. Wote watakaokuwa Jehanamu

Andiko la msingi: Mshahara wa dhambi ni mauti, lakini kalama ya Mungu ni uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu. (Rumi 6:23)

### Simulizi ya Biblia - kupanda mbegu

Tu *tangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi*.

Biblia inatumia mifano ili kufundisha kweli. Mifano ya simulizi ndiyo yenye kuwa na maana na tafsiri mzuri na undani zaidi katika kuelezea kweli ya Mungu. "Mwana wa Adamu" ni jina la Mungu.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

Akawatolea mfano mwingine, akisema, "ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake; lakini watu walipo lala akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake.Baadaye kajani ya ngano yalipomea na kuzaa, yakaonekana na magugu. watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema kwenye konde lako? Limepata wapi basi magugu? akawaambia adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, basi, wataka twende tukayakusanye? Akasema la; msije mkakusanya magugu na kuzing'oa ngano pamoja nayo. Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, yakusanyeni kwanza magugu, muyafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu."akajibu, akasema, azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu; lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu; yule adui aliye yapanda ni Ibilisi. mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika. Basi kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia. Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kuotoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi. na kuwatupa katika tanuru ya moto. ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. ndipo wenye haki watapo ng'ara kama jua katika ufalme wa Baba yao. mwenye masikio na asikie" (Mathayo 13:24-30, 37-43)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Ufunuo 20:12-15; Ufunuo 21-22; 1 Thessalonike 4:13-18; Yohana 14:1-3; Wafilipi 3:20; Mathayo 13:47-50; Mathayo 25:31-46; Marko 9:47-48; Waebrania 9:27)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO - Mungu atahukumu watu wote baada ya kifo. Minguni ni mahali penye maisha tele na furaha. Jehanamu ni mahali penye mateso na maombolezo.

# YESU KRISTO

## Mungu kamili na Mwanadamu Kamili

SOMO 1-8

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Katika Biblia yote Mungu anafanya mpango wa ukombozi ili kuweka njia ya kuurejesha uhusiano uliovunjikakati ya Mungu na wanadamu. Muda ulipotimia Mungu alimtuma mwanawe Yesu Kristo kuwapatanisha wanadamu na Mungu.

Andiko la msingi: Kwa hiyo, Bwana mwenyewe atawapa ishara.Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Emanueli (Isaya 7:14)

### Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Biblia inatuambia kwamba Yesu alikuja kupitia uzao wa Daudi ambao ulikuja kupitia Ibrahimu.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi, Mariamu mama yake, alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana alionekana anamimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye Yusufu mwanawe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu mwana wa Daudi usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na Dhambi zao. Hayo yote yamekuwa ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema, Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana nao watamwita jina lake Emanueli; yaani Mungu pamoja nasi. Naye Yusufu alipoamka katika usingizi alifanya haya malaika wa Bwana alivyomwagiza, akamchukua mkewe; asimjue kamwe hata alipomzaa mwanawe akamwita jina lake Yesu. (Mathayo 1:18-25)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI -Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Mathayo 16:13-20; Mathayo 26:63-64; Luka 1:28-35; Yohana 1:1-14; Yohana 3:16; Waphilipi 2:5-11; Wakorintho 1:15-20; Wakorintho 2:9)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo3:16-17)

===HITIMISHO - Yesu akristo alikuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili.
Yesu akristo alitumwa kuupatanisha uhusiano uliovunjika kati ya Mungu na wanadamu.

# MPANGO WA MUNGU WA UPATANISHO NA WANADAMU

SOMO 1-9

Kuchukua Adhabu Kwaajili Ya Dhambi na Kurudisha Uhusiano

## KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Mungu anawapenda wanadamu wote. Wanadamu waliumbwa kumpenda Mungu na kuwa nauhusiano na Mungu. Shetani aliwashawishi Adamu na Eva kumwasi Mungu. Kumwasi Mungu ni dhambi. Dhambi iliharibu uhusiano mkamilifu kati ya Mungu na mwanadamu. Mungu alimwahidi mwanadamu kuwa uhusiano mkamilifu kati ya Mungu na mwanadamu utarejeshwa. Mungu alimuahidi Adamu kuwa siku moja, mmoja kutoka kwenye uzao wake atakiponda kichwa cha Shetani. Mungu aliahidi kuwa atayabariki mataifa ya dunia, kupitia uzao wa Ibrahumu. Mungu alitimiza ahadi zake kwa kumleta mwanawe Yesu Kristo.

Andiko la msingi: Kwamaana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia Kristo alikufa kwaajili ya waovu. (Warumi 5:6)

## Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi*.

Mungu alimleta mwanawe wa pekee jina lake Yesu Kristo. Alizaliwa kwa muujiza. Alikuwa Mungu na mwanadamu. Aliishi nakukua na hakuwahi kutenda dhambi.alifanya miujiza mingi na alifundisha wengi kwa hekima. Wakuu wengu wa dini hawakumpenda Yesu na waazimia kumwua. Mtawala mkuu alimhoji Yesu, na kumwona kuwa hakuwa na hatia. Ili kuwaridhisha makutano mtawala aliwaruhusu watu kumpiga Yesu, na kumsulibisha msalabani. Msalaba kilikuwa chombo cha mateso. Mungu alisema ni kwa sababu ya dhambi zetu, Yesu alipigwa na kuuwawa.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

ndipo askari wa Walawi akamchukua Yesu ndani ya Praitorio, wakamkusanyia kikosi kizima. Wakamvua ngua wakamvika vazi jekundu. Wakasokota taji ya miiba, wakaiweka juu ya kichwa chake na mwanzi katika mkono wake wa kuume; wakapiga magoti mbele yake, wakamdhihaki, wakisema, salamu mfalme wayahudi! Kasha wakamtemea mate, na kuutwaa ule mwanzi wakampiga piga kichwani. Walipokwisha kumdhihaki, wakalivua lile vazi, wakamvika mavazi yake, wakamchukua kumsulibisha. Hata walipokuwa wakitoka wakamwona mtu mkirene, jina lake Simoni, huyu wakamshurutisha auchukue msalaba wake, na walipofika mahali paitwapo Golgotha, yaani fuvu la kichwa, wakampa kunywa divai iliyochanganyika na nyongo; lakini yeye alipoionja hakutaka kunywa. Walipokwisha kumsulibisha waligawa mavazi yake wakapiga kura, (ili litimie neno lililonenwa na nabiiwaligawa nguo zangu kati yao, na juu ya vazi langu walipiga kura), wakaketi wakamlinda huko. Wakaweka juu ya kichwa chake mashitaka yake yaliyoandikwa HUYU NI YESU MFALME WAYAHUDI. Wakati uo huo wanyang'anyi wawili wakasulibishwa pamoja naye, mmoja mkono wake wa kuume na mmoja mkono wake wa kushoto. Basi tangu saasita palikuwa na giza juu ya nchi yote hata saa tisa. Naye Yesu akiisha kupaza sauti yake tena kwa nguvu, akaitoa Roho yake (Mathayo 27:27-38, 45, 50)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(1 Timotheo 1:15; 1 Petro 2:24; Marko 10:45; Waefeso 1:7; Yohana1:29; Isaya 53:5-6)

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo3:16-17)

===HITIMISHO - Kifo cha Yesu Kristo msalabani kilifanya njia kwa watu wote, kuwa na uhusiano maalumu na Mungu. Yesu alilipa gharama yote ya dhambi zetu. Yesu alikuwa dhabihu kamili ya mara moja kwaajili ya dhambi. Yesu alichukua nafasi yetu. Hatukugharamia zawadi hii maalumu, Mungu alifanya hivi kwa sababu anawapenda watu wote. Wale wanaomwamini Yesu Kristo na kupokea zawadi ambayo Yesu Kristo ameitoa wanapatanishwa na Mungu.

# YESU ANASHINDA MAUTI

SOMO 1-10

## Kufufuka Kwake Kunadhihirisha Alikuwa Nani

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Alipokuwa hapa duniani, Yesu alisema atakufa kwaajili ya dhambi zetu, na kufufuka katika wafu. Yesu Kristo alikufa msalabani na baadaye akaurudia uhai. Yesu Kristo alipofufuka katika kwa wafu, alithibitisha kuwa alikuwa Mungu kweli. Yale aliyoyasema na kuamuru ni kweli.

Andiko la msingi: Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe fyakuwa Kristo alikufa kwaajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko na kuwa alizikwa, na kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko; (1 Wakorintho 15:3-4)

### Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi*.

Baada ya kifo cha Yesu msalabani baadhi ya marafiki, waliuchukua mwili wake. Walimzika Yesu katika kaburimtawala akaamuru jiwe kubwa liwekwe kwenye mlango wa kaburi. Askari walilinda kaburi kuzuia watu wasiuibe mwili wa Yesu. siku ya tatu baada ya kifo chake wanawake wawili walikwenda kaburini. Walikuta jiwe lile limeviringishwa na malaika amekaa juu yake

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-
Malaika akajibu, akamwambia, wale wanawake, msiogope ninyi, kwa maana najua ya kuwa mnamtafuta Yesu aliyesulibiwa. Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema, njoni mpatazame mahali alipolazwa nanyi nendeni upesi mkawaambie wanafunzi wake, amefufuka katika wafu. Tazama awatangulia kwenda galilaya; ndiko mtakakomwona. Haya nimekwisha waambia. Wakaondoka upesi kutoka kaburini, kwa hofu na furaha nyingi, wakaenda mbio kuwapasha wanafunzi wake habari. (Mathayo 28:5-8)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(1 Wakorintho15:12-22; Warumi1:3-4; Warumi 8:33-34; Matendo 2:22-24; 1 Petro1:3)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo3:16-17)

===HITIMISHO - Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, kifo hakikuweza kumdhibiti Yesu Kristo kwa sababu yeye ni Mungu. Alikuwa dhabihu kamilifu kwaajili ya dhambi. Yesu Kristo ni Mungu wa uzima. Yesu Kristo alithibitisha kuwa hakuwa tu mwalimu au nabii. Yesu Kristo alithibitisha alikuwa na nguvu zote na mamlaka. Yesu Kristo alithibitisha kuwa ni mfalme wa ulimwengu.

# NIFANYE NINI ILI NIPATE KUOKOKA?

SOMO 1-11

Amini

## KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Yesu alikufa na kufufuka katika wafu ili watu wawe na uzima. Watu wote wameitwa kumwamini Yesu na kuamini kuwa ni mwana wa Mungu. Watu wote wanaweza leo kuokoka na adhabu ya dhambi kama wakimwamini Yesu na kukiri kwa kinywa chao kuwa ni Mungu wau wote wana uchaguzi kumwamini Mungu na kuokoka au kumkataa. Mungu anataka watu wote waokoke.

Andiko la msingi: Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye, asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye (Yohana 3:16-17)

## Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Baada ya Yesu kufufuka katika wafu aliwatokea wafuasi wake. Mmoja wa wafuasi wake aliyeitwa Tomaso, hakuwa pamoja na wenzake, hakumwona Yesu tangu aliposulibiwa kuamini kitu kuwa ni cha uhakika bila kukiona au kukigusa inaitwa imani.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

Walakini mmoja wa wale thenashara Tomaso, aitwae pacha, hakuwako paoja nao alipokuja Yesu, basi wanafunzi wengine wakamwambia, tumemwona Bwana. Akawaambia mimi nisipoziona mikononi mwake kovu za misumari, na kutia kidole changu katika mahali pa msumari na kutia mkono wangu katika ubavu wake, mimi sisadiki hata kidogo. Basi baada ya siku nane, wanafunzi wake walikuwao ndani tena na Tomaso pamoja nao. Akaja Yesu na milango imefungwa, akasimama katikati akasema, amani iwe kwenu, kasha akamwambia Tomaso, lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu, ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye. Tomaso akajibu akamwambia Bwana wangu na Mungu wangu; Yesu akamwambia wewe kwa kuwa umeniona umesadiki; wa heri wale wasioona wakasadiki.
Basi kuna ishara nyingine nyingi ambazo yesu alizifanya mbele ya wanafunzi wake, zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, mwana wa Mungu na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake (Yohana 20:24-31)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Waefeso 2:8-9; Wagalatia 2:20; Wagalatia 3; Matendo 10:43; Matendo16:25-31; Waebrania 11; Warumi 6:23; Warumi 10:9-10; Yohana 3:16-21)

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO - Yesu Kristo aliichukua adhabu ya dhambi zetuMaandiko yanasema watu watakuwa na uzima wa milele wakiamini kuwa Mungu alimfufua katika wafu. Haiwezekani kuwa mkristo bila imani. Imani ni kumwamini na kumtumaini Yesu, hata kama hatumwoni. Imani ni kuamini kuwa Yesu Kristo alifufuka katika wafu kukabili dhambi zetu.

# TUNAITIKIAJE UPENDO WA MUNGU?

SOMO 1-12

## Tubu

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Kutubu ni badiriko la moyo na mawazo. Toba inajumuosha kuwaza na kutenda tofauti juu ya dhambi na Mungu. Toba maana yake tunaichukia dhambi, kama Mungu anavyoichukia dhambi. Toba inasababisha mabadiriko ya tabia, na kutenda dhambi.

Andiko la msingi: zamani zile za ujinga, Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaangaza watu wa kila mahali watubu. (Acts 17:30)

### Simulizi Ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu alikuwa mwalimu hodali na alifanya miujiza mingi, na aliwaponya wenya mahitaji. Popote Yesu alipokwenda alikuwa na maundi makubwa.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

"Naye alipoingia Yeriko alipita katikati yake. Na tazama palikuwa na mtu, jina lake zakayo, mkubwa mmoja katika watoza ushuru naye Tajiri. Huyu alikuwa akitafuta kumwona Yesu, ni mtu wa namna gani, asiweze kwa sababu ya umati wa watu, maana ni mfupi wa kimo. Akatangulia mbiyo akapanda juu ya mkuyu apate kumwona, kwa kuwa atakuja kuipitia njia ile. Na Yesu alipofika mahali pale, alitazama juu akamwambia, Zakayo, shuka upesi kwa kuwa leo imenipasa kushinda nyumbani mwako. Akafanya haraka, akashuka, akamkaribisha kwa furaha. Hata watu walipoona, walinung'unika wote,, wakisema, ameingia kukaa kwa mtu mwenye dhambi. Zakayo akasimama, akamwambia Bwana , tazama, Bwana, nusu ya mali yangu nawapa maskini, na ikiwa nimemnyang'anya mtu kitu kwa hilanamrudishia mara nne. Yesu akamwambia, leo wokovu umefika nyumbani humu, kwa sababu huyu naye ni mwana wa Ibrahimu. Kwa kuwa mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea." (Luka 19:1-10)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Matendo 2:31-41, Matendo3:19-20; Mathayo 3:2; Mathayo 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; Luka 13:15)

### MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO - Imani yetu kwa Yesu inatupelekea kutubu. Tunapotubu, mioyo na mawazo yetu yanabadirishwa. Mioyo na mawazo yetu yanapobadirishwa, tabia zetu za dhambi zinabadirika. Wale wanaomwamini na kumtumaini Yesu wanaishi tofauti na wale wanaowazunguka wasiomwamini na kumtumaini Yesu .

# MIMI NI RAFIKI WA BWANA YESU

SOMO 1-13

## Nabaki katika Upendo wake kwa kutii Amri zake

### KIINI CHA SOMO - Kuandaa Udongo

Kama wafuasi wa Yesu sisi pia ni marafiki wa Mungu. Marafiki wa Mungu qanamjua Mungu katika hali ya upekee. Marafiki wa Mungu wanampenda Mungu, na wanawapenda watu wengine. Marafiki wa Mungu wanamwamini Mungu na kutii amri zake.

Andiko la msingi: kondoo wangu wanaisikia sauti yangu, ninawajua nao wananifuata. (Yohana 10:27)

### Simulizi ya Biblia - kupanda mbegu

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu anasema na mitume wake akiwaelekeza. Baba anayemzungumzia ni Mungu baba.

Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-

Filipo alimwambia Bwana utuonyeshe Baba yatutosha. Yesu akamwambia, mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje utuonyeshe Baba?

Kama vile Baba alivyo nipenda mimi, nami nalivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu,mtakaa katika pendo langu kama mimi nilivyozishika amri za Baba yangu, na kukaa katika pendo lake. Hayo nimewaambia ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimilizwe. Amri yangu ndi hii, mpendane kama nilivyowapenda ninyi. Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwaajili ya rafiki zake. Nanyi mmekuwa rafiki zangu, mkitenda niwaamuruyo. Siwaiti tena watumwa, kwa maana mtumwa hajui atendalo Bwana wake; lakini ninyi nimewaita rafiki, kwa kuwa yote niliyoyasikia nimewaarifu." (John 14:8-9; 15:9-15)

### MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

### MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - Kupunguza

(Mathayo 7:16-20; 2 Petro 1:3-8; Yohana 14:15-23; 1 Yohana 4:7-8; 1 Yohana5:1-5; Wakorintho 1:10)

### MAOMBI NA MASWALI/MSING -Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16-17)

===HITIMISHO - Kama wafuasi wa Yesu, sisi ni rafiki wa Mungu tumeitwa kuisikia sauti ya Mungu na kutii kama marafiki wa Mungu, tumeitwa tuwapende wengine kama vile Yesu anavyotupenda sisi.

iBFAM

www.iBFAM.org

KUZAA NA KUONGEZEKA



# KAENI NDANI YA KRISTO

Mpangilio wa Masomo! 2 *Msingi*

*"Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu.". (Yohana 15:4)*

# *Msingi*

## Mpangilio wa pili wa somo: *Ukrasa*

**Masomo:**


2-1 Kubatizwa: ....................................34
Kumwamini Bwana Mungu

2-2 Sisi ni nuru ya Ulimwengu: ....................................35
uambiye ulimwengu Yesu ni nani?

2-3 Kupatanishwa na Wengine: ....................................36
wasamehe wote waliokukosea (kutenda dhambi)

2-4 Usizini (Usifanye zinaa): ....................................37
usiangalie na kuwa na mtazamo kama wa wenginge kwa habari ya zinaa

2-5 Ndoa ni dhabihu kwa Mungu: ....................................38
Mungu hapendi kuachana katika ndoa

2-6 Kukubali katika Haki: ....................................39
Kuishi kwa mfano wa upendo, upendo wa Mungu.

2-7 Wapende adui zako: ....................................40
Mungu anawapenda watu wote

2-8 Toa kwa Wengine (Utoaji): ....................................41
Mungu huwajali wenye mahitaji

2-9 Maombi: ....................................42
kuomba pamoja na kumsikiliza Mungu

2-10 Weka akiba (hazina) yako Mbinguni: ....................................43
kumheshimu Mungu kwa kaisha na kali zetu

2-11 Usiogope: ....................................44
Mungu anajua na anajali mahitaji yako

2-12 Usihukumu wengine: ....................................45
Mungu ndiye hakimu

2-13 Ombeni, tafuteni, na bisheni: ....................................46
Mungu huyakubali maombi ya mtu aliyejishusha

# KUBATIZWA (Ubatizo)

SOMO 2-1

*Kuamini katika Mungu (i.e. Kumwamini Mungu)*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Ubatizo wa maji ni agizo kutoka kwa Mungu. Biblia inasema kwamba baada ya kumpokea Kristo, lazima kubatizwa. Kubatizwa ni pale waamini katika Kristo wanapozamishwa katika maji na kutolewa. Ubatizo ni picha ya kuzaliwa kiroho ambayo inatokea pale tunapokuwa wakristo. Ubatizo ni picha kwa wengine kwamba tunamfuata Kristo.

**Andiko la Msingi**: "***Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu.***" **(Mt. 28:19)**

## Simulizi ya Biblia - Kupanda mbegu

**Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi**. Kwa hiyo, Filipo alikuwa ni MFUASI wa Kristo Yesu ambaye alitangaza habari njema za ufalme wa Mungu kwa watu wote.

**Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-**

"*Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo pamoja na makutano kwa nia moja wakasikiliza maneno yale yaliyosemwa na Filipo. Walipoyasikia na kuziona ishara alizokuwa akizifanya, kwa maana pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao, wakiliza kwa sauti kuu, na watu wengi waliopooza, na viwete wakaponywa. Ikawa furaha kabisa katika mji ule. Na mtu mmoja jina lake Simoni, hapo kwanza alikuwa akifanya uchawi katika mji ule, akawashangaza watu wa taifa la Samaria, akisema ya kuwa yeye ni mtu mkubwa. Wote wakamsikiliza tangu mdogo hata mkubwa, wakisema, mtu huyu ni uweza wa Mungu ule mkuu. Wakamsikiliza kwa maana amewashangaza muda mwingi kwa uchawi wake. Lakini walipomwamini Filipo,akazihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo wakabatizwa, wanaume na wanawake. Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka.*" (Mdo 8:5-13)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - Maji na rutubisha

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA: - Kupunguza:

*(Matendo 2:38; Matendo 18:8; Rumi 6:4-5; Kolosai 2:12; Galatia 3:27)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - Kuvuna Matunda (2 Timotheo 3:16)

**====HITIMISHO:** - Biblia inasema kwamba, mtu baada ya kuzaliwa mara ya pili na kuwa Mkristo ni lazima abatizwe; na ubatizo wa maji ni picha au alama inayoonyesha picha ya kitu gani au ni nini kinachochukua nafasi katika mioyo yetu pale tunapompokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi. Ubatizo ni shuhuda kwa wengine kwamba tunamfuata Yesu Kristo

# SISI NI NURU YA ULIMWENGU

SOMO 2-2

*Uambie Ulimwengu Yesu Kristo ni Nani!*

## KIINI CHA SOMO - *Kuanda udongo*

Mkristo ni mtu anayemfuata Yesu Kristo. Maandiko yanasema kwamba Mkristo awe au anatakiwa nuru ya ulimwengu ili apate kumfunua Yesu Kristo ni nani.

**Andiko la Msingi**: *"Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango, nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema wamtukuze baba yenu aliye mbinguni"* (Mt. 5:14-16)

## Simulizi ya Biblia - *Panda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa simulizi za Yesu Kristo!*

Wakati alipokuwa amekaa pale kisimani, mwanamke akaja kuchota maji, Yesu akamuomba maji ili anywe. Yesu Kristo akamwambia yule mwanamke kuwa atampa maji ya uzima wa milele. Yesu akajifunua na akajidhihirisha kwa yule mwanamke kwamba yeye ni Mungu. Mwanamke yule alishangazwa na maneno yale ya Yesu na kuamini yote aliyosema.

Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-

***"Basi yule mwanamke akauacha mtungi wake akaenda zake mjini, akawaambia watu. Njoni, mtazame mtu aliyeniambia mambo yote niliyoyatenda. Je! Haimkini huyu kuwa ndiye Kristo? Basi wakatoka mjini, wakamwendea. Na katika mji ule wa Samaria wengi walimwamini kwa sababu ya neno la yule mwanamke, aliyeshuhudia kwamba, aliniambia mambo yete niliyoyatenda. Basi wale wasamaria walipomwendea, walimsihi akae kwao naye akaa huko siku mbili. Watu wengi zaidi wakaamini kwa sababu ya neno lake. Wakamwambia yule mwanamke sasa tunaamini wala si kwa manebno yako tu, maana tumesikia wenyewe, tena twajua hakika huyu ndiye mwokozi wa ulimwengu"*. (Yohana. 4:28-30,39-42)**

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Matendo 1:8; Marko 16:15-16; Luka 11:33-36)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16)*

**====HITIMISHO:** - Yesu ni nuru ya kweli na mwokozi wa ulimwengu. Yesu aliwaambia wafuasi wake (Wanafunzi) enendeni na mkawe nuru ya ulimwengu, ili ulimwengu upate kuona kuwa nuru ya kweli ambayo ni (Yesu Kristo).

# KUPATANISHWA NA WENGINE

SOMO 2-3

***Wasamehe wote waliokukosea (kutenda dhambi)***

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Yesu anawafundisha wanafunzi wake kuishi kwa amani na kila mtu. Wakristo wanafundishwa kuwa na huruma na kila mtu na kuwarehemu wote wanaowatenda dhambi. Kuishi kwa amani na kila mtu ni kuonyesha hali ya kusamehe wote wanaokukosea.

Andiko la Msingi: ***"....Basi ukileta sadaka yako madhabahuni na huku ukikumbuka kuwa ndugu yako ana neno juu yako iache sadaka yako mbele ya madhabahu uende zako ukapatane kwanza na ndugu yako kasha urudu uitoe sadaka yako"*** **(Mt. 5:23-24)**

## Simulizi ya Biblia - *Panda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa simulizi za Yesu Kristo kwa Wanafunzi.*

Hivyo, wanafunzi wake walimuuliza BWANA Yesu Kristo ni mara ngapi anatakiwa kuwasamehe watu waliomkosea, katika kujibu Yesu alimwambia maneno yafuatayo:-

**Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-**

***"Kwa sababu hii, ufalme wa mbinguni umefanana na mfalme mmoja aliyetaka kufanya hesabu na watumwa wake. Alipoanza kuifanya aliletewa mtu mmoja awiwaye talanta elfu kumi. Naye alipokosa cha kulipa Bwana wake akaamuru auzwe, yeye na mkewe na watoto wake, na vitu vyote alivyo navyo ikalipwe ile deni. Basi yule mtumwa akaanguka akamsujudia akisema, Bwana, nivumiliye nami nitakulipa yote pia. Bwana wa mtumwa yule akamhurumia, akamfungua akamsamehe ile deni. Mtumwa yule akatoka akamwona mmoja wa wajoli wake, aliyemwia dinari mia akamkamata akamshika koo, akisema nilipe uwiwacho. Basi mjoli wake akaanguka miguuni pake akamsihi akisema, nivumiliye nami nitakulipa yote pia. Lakini hakutaka akaenda akamtupa kifungoni, hata atakapoilipa ile deni. Basi wajoli wake walipoyaona yaliyotendeka, walisikitika sana wakaenda wakamweleza Bwana wao yote yaliyotendeka ndipo Bwana wake akamwita, akamwambia, ewe mtu mwovu, nalikusamehe wewe deni yote, uliponisihi nawe je! Haikukupasa kumrehemu mjoli wako kama mimi nilivyokurehemu wewe? Bwana wake akaghadhibika, akampeleka kwa watesaji, hata atakapoilipa ile deni yote. Ndivyo na Baba yangu wa mbinguni atakavyowatenda ninyi msiposamehe kwa mioyo yenu kila mtu ndugu yake".*** **(Mt. 18:23-35)**

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Mathayo 6:14; Luka 11:4; 17:3-4; 2 Wakorintho 2:5-11; Kolosai 3:12-14; Wafeso 4:32; Marko 11:25-26)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO** - "....Wafuasi (wanafunzi) wa Yesu aliitwa ili wapate kuwasamehe watu wengine wanaowakosea kama vile ambavyo Mungu anavyowasamehe. Hivyo, wafuasi wa Yesu wanaongozwa ili wapate kuishi maisha ya amani na watu wote wanaowazunguka."

# USIZINI
# (USIFANYE ZINAA)

SOMO 2-4

*Usiangalie/Kuwa na mtazamo kama wengine wa zinaa*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Yesu anawafundisha wanafunzi wake wasizini. Yesu anafundisha kwamba kwa kuangalia mtu na kumtamani umekwisha kuzini/kutenda dhambi moyoni mwako.

Andiko la Msingi: ***"..Mmesikia kwamba imenenwa usizini, lakini mimi nawaambia, kila mtu atamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake"*** **(Mt. 5:27-28)**

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Daudi alikuwa mfalme maarufu wa Israel. Daudi alimwona mwanamke akiwa anaoga na kumtamani. Mwanamke huyo alikuwa ni mke wa kamanda wa jeshi la Daudi. Mtu huyo alikuwa anaitwa Uriah. Daudi aliwataka watumishi wake wamlete yule mwanamke. Daudi alimpa mimba yule mwanamke. Alimtuma Uriah kwenda kupigana vita na Uria alikufa vitani. Mungu alifedheheshwa akamtuma nabii aliyeitwa Nathani kwenda kwa Daudi.

**Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-**

*"Ndipo Bwana akamtuma Nathani aende kwa Daudi, Nathani akamwendea, akamwambia,palikuwa na watu wawili katika mji mmoja, mmoja wao alikuwa tajiri, wa pili maskini. Yule tajiri alikuwa na kondoo na ng'ombe wengi sana, bali Yule maskini hakuwa na kitu, ila mwanakondoo mmoja mdogo ambaye amemnunua na kumlea, naye akakua pamoja naye na pamoja na wanawe, hula sehemu ya posho lake na kukinywea kikombe chake, na kulala kifuani mwake, akawa kwake kama binti. Hata msafiri mmoja akamfikia Yule tajiri naye akaacha kutwaa moja ya kondoo zake mwenyewe, au mmoja wa ng'ombe zake mwenyewe, ili kumwandalia Yule msafiri aliyemfikilia bali alimnyang'anya Yule maskini mwanakondoo wake, akamwandalia Yule mtu aliyemfikilia. Ndipo hasira ya Daudi ikawaka sana juu ya mtu Yule, akamwambia Nathani aishivyo Bwana mtu huyo aliyetenda jambo hili,hakika yake astahili kufa naye atamrudishia Yule mwanakondoo mara nne, kwasababu ametenda neno hili na kwa sababu hakuwa na huruma. Basi Nathani akamwambia Daudi wewe ndiwe mtu huyo, Bwana Mungu wa Israel asema hivi nalikutia mafuta uwe mfalme juu ya Israel nikakuokoa na mkono wa Sauli, name nikakupa nyumba ya Bwana wako na wake za Bwana wako kifuani mwako, nikakupa nyumba ya Israel nay a Yuda na kama hayo yangalikuwa machache ningalikuongezea mambo kadha wa kadha. Kwa nini umelidharau neno la Bwana? Na kufanya yaliyo mabaya machoni pake? Umempiga Uriah Mhiti, kwa upanga, nawe umemtwaa mkewe awe mke wako, nawe umemuua huyo kwa upanga wa wana wa Amoni"* (2 Sam 12:1-9)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Kutoka 20:14; Waebrania 13:4; Waefeso 5:3-5; 1 Wakorintho 6:13-20; Wakolosai 3:1-11; 1 Thessalonike 4:3-8; Mithali 6:32)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO:** - Uzinzi unafanywa na wale ambao siyo waaminifu katika mahusiano katika ndoa. Usinzi na dhambi machoni pa Mungu. BWANA Yesu aliwaambia wanafunzi (wafuasi) wake wasifanye (wasizini). Vivyo hivyo, akafundisha kule kuwa na mawazo ya zinaa (kumtamani mwanamke/mwaume ili ufanye naye uzinzi ni dhambi iliyofanywa tayari moyoni).

# NDOA NI DHABIHU KWA MUNGU

SOMO 2-5

*Mungu hapendi kuachana katika ndoa*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Yesu anafundisha uhusiano wa ndoa ni sadaka na pia uhusiano huo ni wa muhimu sana kwa Mungu.

Andiko la Msimgi: ***"Lakini mimi nawaambia, kila mtu amwachaye mkewe, isipokuwa kwa habari ya uasherati amfanya kuwa mzinzi, na mtu akimuoa yule aliye achwa azini."*** **(Mt. 5:32)**

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Kundi kubwa la watu lilimfuata Yesu kwa sababu alikuwa anaponya watu. Mafarisayo walikuja kwa Yesu na kumuuliza maswali mengi. Mafarisayo walikuwa ni viongozi wa dini katika dini ya kiyahudi. Mafarisayo walifuata sheria nyingi za dini ambazo, Mungu alimpa Musa. Musa alikuwa ni mtu aliyewaongoza wana wa Israel kabla ya Yesu kuzaliwa.

Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:- "*Basi, Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, wakamwambia, je ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu? Akajibu akawaambia, je! Hamkusoma yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke? Akasema, kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu mwanadamu asiwatenganishe. Wakamwambia, jinsi gani basi, Musa aliamuru kumpa hati ya talaka na kumwacha? akawaambia, Musa kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu, aliwaparuhusa kuwaacha wake zenu, lakini tangu mwanzo haikuwa hivi.*" (Mt.19:3-9)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Waefeso 5:21-28; Mwanzo 2:20-24; 1 Wakorintho 7)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* (2Timotheo. 3:16-17)

**====HITIMISHO** - Ndoa iliumbwa na kuasisiwa na Mungu. Hivyo, dhabihu kwa BWANA Mungu. Kwa msingi huo, wafuasi wa Yesu wanatakiwa kufanya kila linalowezekana sawa na mapenzi ya Mungu wapate kulizilinda ndoa zao.

# KUKUBALI KATIKA HAKI

SOMO 2-6

*Kuishi kwa mfano wa Upendo, Upendo wa Mungu*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo.*

Yesu anafundisha wanafunzi wake jinsi ya kukubali pale unapoonewa. Yesu anawaambia wanafunzi wake wasilipize kisasi kwa mtu aliyewakosea. Yesu anasema wakristo waishi kwa mfano wa upendo na upole kwa watu wote.

Andiko la Msingi: ***“Lakini mimi nawaambia msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili, na mtu atakaye kukushitaki na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia, na mtu atakayekulazimisha mwendo wa maili moja, nenda naye mbili, akuombaye mpe, naye atakaye kukopa kwako usimpe kisogo.”*** **(Mathayo. 5:39-41)**

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu.*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Yuda ni mmoja wa wanafunzi wa Yesu. Viongozi wa dini walitaka kumuua Yesu. Yuda alimsaliti Yesu kwa pesa katika simulizi hii. Yesu alikuwa akiongea na wanafunzi wake isipokuwa Yuda. Yesu alijua kuwa Yuda atakuja kumsaliti.

Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:- “***basi alipokuwa katika kusema, tazama mkutano wa watu, na yule aitwae Yuda ambaye ni mmoja wa wale thenashara, amewatangulia. Akamkaribia Yesu ili kumbusu. Yesu akamwambia, Yuda, wamsaliti mwana wa Adamu kwa kumbusu? na wale waliokuwa karibu naye walipoona yatakayotukia, walisema Bwana tuwapige kwa upanga? mmoja wao akampiga mtumwa wa kuhani mkuu, akamkata sikio la kuume. Yesu akajibu akasema mwe radhi kwa hili. Akamgusa sikio akamponya. Yesu akawaambia wakuu wa makuhani, na maakida wa hekalu, na wazee waliokuja juu yake, je! Mmekuja wenye panga na marungu kama kumkamata mnyang'anyi? Kila siku nilipokuwa pamoja nanyi hekaluni, hamkuinyoshea mikono, lakini hii ndiyo saa yenu na mamlaka ya giza.***” **(Luka. 22:47 - 53)**

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Luka 6:32; Waefeso 5:1-2; Warumi 12:17-21; Yohana 4:7-8; 13:34; Marko 12:28-31; 1 Petro 1:22; 1 Yohana 3:11; 1 Wakorintho 4:12; 1 Petro 3:9; 2 Wakorintho 12:10)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2Tim. 3:16-17)*

**====HITIMISHO** - "......Yesu aliwaambia wanafunzi wake wasilipize kisasi kwa watu waliowakosea. Wafuasi wa Kristo walikubali toauti na matatizo zaidi ya watu wengine kwa sababu walijua upendo wa Yesu. Yesu alisema wakristo waishi kama mfano mzuri wa upendo na upole kwa watu wote."

# WAPENDE MAADUI ZAKO

SOMO 2-7

*Mungu anawapenda watu wote*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuwapenda na kuwaombea maadui zao. Yesu anasema kwamba ni vigumu kuwapenda watu waliokutenda vibaya. Yesu anawaambia wanafunzi wake kuwa wao wako tofauto na wengine kwa sababu wanatakiwa kuwapenda wote.

Andiko la Msingi: ***"....Lakini mimi nawaamimbia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na .....; huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki." (Mathayo. 5:44-45)***

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Wakati Yesu anaishi ulimwenguni, alikuwa na adui wengi sana. Maadui hawa walimchukia Yesu. BWANA Yesu Kristo aliumizwa na hata kuuwawa na adui zake.

**Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-**

"*Na walipokuwa wakimwondoa walimkamata mtu mmoja, Simoni mkirene, aliyekuwa ametoka shamba, wakamtwika msalaba, auchukue nyuma yake Yesu. Wakapelekwa na wawili wengine wahalifu wauawe pamoja naye. Na walipofika mahali paitwapo fuvu la kichwa, ndipo walipo msulibisha yeye na wale wahalifu, mmoja upande wa kuume na mmoja upande wa kushoto. Yesu akasema Baba (MUNGU) uwasamehe kwa sababu hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake, wakapiga kura. Watu wakasimama wakitazama, wale wakuu nao walikuwa wakimfanyia mzaha wakisema, aliokoa wengine, na ajiokoe mwenyewe, kama ndiye Kristo wa Mungu mteule wake. Wale askari nao wakamfanyia dhihaka, wakimwendea na kumletea siki, huku wakisema kama wewe ndiwe mfalme wa wayahudi, ujiokoe mwenyewe. Na juu yake palikuwa na anuani; Huyu ndiye Mfalme wa Wayahudi. Na mmoja wa wale wahalifu waliomtundika alimtukana, akisema je! Wewe ni Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini Yule wa pili akamjibu, akamkemea, akisema, wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi, kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu, bali huyu hakutenda lolote lisilofaa. Kisha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako. Yesu akamwambia, amini nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi.*" (Luka. 23:26-27,32-43)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Marko 12:28-31; Yohana 13:34; Rumi 12:17-21; Luka 6:27-38)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2Timotheo. 3:16-17)*

**====HITIMISHO** - Yesu anatufundisha kuwapenda na kuwaombea wale wote wanaotukosea. BWANA Yesu Kristo anaonyesha kuwarehemu wale wote waliomkosea na kumuua. Wafuasi wa Kristo kuwakubali adui zao kama Yesu alivyofanya.

# TOA KWA WENGINE (UTOAJI)

SOMO 2-8

*Mungu huwajali wenye mahitaji*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Yesu anawafundisha wanafunzi wake kuhusu kuwajali na kuwasaidia wote wenye mahitaji. Hivyo, wafuasi wa Kristo hawatoi kwa wale wote ambao wamewazunguka, bali kwa wale wenye uhitaji.

Andiko la Msingi: ***"Amini nawaambieni, wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe utoapo sadaka hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wako wa kuume; sadaka yako iwe kwa siri; na Baba yako aonaye sirini atakujazi"*** **(Mathayo.6:3-4)**

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Wanafunzi wa Yesu walimuuliza Yesu kuhusu nini kitatokea mwisho wa dunia. Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba mwisho wa dunia atakuwa mfalme, na kuwahukumu watu wote

**Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-**

"*Na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi; atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto. Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, njoni mliobarikiwa na Baba yangu , urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika; nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia. Ndipo wenye haki watamjibu wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni tukakujia? Na mfalme atajibu, akiwaambia, amini, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmoja wapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi. Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu; msininyweshe; nalikuwa mgeni msinikaribishe; nalikuwa uchi; msinivike; nalikuwa mgonjwa na kifungoni; msije kunitazama. Ndipo hao pia watajibu, wakisema Bwana, ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? Naye atawajibu akisema, Amini nawaambia kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi. Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakuwa katika uzima wa milele*" (Mathayo. 25:32-46)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Mithali .19:17; 28:27; Zaburi. 82:3; Mathayo .5:42; 19:21; Yeremia. 22:3)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO** - Yesu anawajali wenye kuwa na uhitaji. Hivyo, anawafundisha wafuasi wake, kuwapa wanaohitaji. Yesu atawatunuku wale wote wanaotoa kwa wahitaji.

# MAOMBI

*Maombi pamoja na Kumsikiliza*

SOMO
2-9

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Yesu anawafundisha wanafunzi wake kuwa wanatakiwa waombe kila mara. Maombi ni kuongea na Mungu na kusikiliza kutoka kwa Mungu. Hivyo, tunapoomba Mungu hutusikia.

Andiko la Msingi: *"**Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani. Na ukisha kufunga mlango wako usali mbele za Baba yako aliye sirini, na Baba yako aonaye sirini atakujazi.**"* **(Mathayo.6:6)**

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Mfalme mmoja aliyeitwa Herode, alikuwa anawachukia Wakristo. Mfalme Herode alianza kuua wote waliokuwa katika kanisa. Askari alimkamata kiongozi wa kanisa aliyeitwa Petro na kwenda kumuua.

**Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-**

*"Basi Petro akalindwa gerezani, nalo kanisa likamwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake. Hata wakati Herode alipotaka kumtoa, usiku ule ule Petro alikuwa amelala katikakati ya askari wawili; walinzi mbele ya mlango wakailinda gereza. Mara malaika wa Bwana akasimama karibu naye, nuru ikamulika mle chumbani, akampiga Petro ubavuni, akamwambia akisema ondoka upesi. Minyororo yake ikamwanguka mikononi. Malaika akamwambia, jifunge ukavae viatu vyako. Akafanya hivyo. Kisha akamwambia jivike nguo zako, ukanifuate. Akatoka nje akamfuata; wala hakujua yakuwa ni kweli yaliyofanywa na malaika; bali alidhani anaona maono. Na walipopita lindo la kwanza na la pili, wakaja hata mlango wa chumba cha kuingilia mjini, ukawafungukia wenyewe. Wakatoka nje wakapita katika njia moja; mara malaika akamwacha. Hata Petro alipopata fahamu akasema, sasa nimejua yakini ya kuwa Bwana amempeleka malaika wake na kunitoa katika mkono wa Herode na katika kutazamia kote kwa taifa la wayahudi. Na alipokuwa akifikiri haya akafika nyumbani kwa Mariamu , mamaye Yohana, ambaye jina lake la pili ni Marko, na watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba. Naye alipobisha kilango cha lango, kijakazi jina lake Roda, akaja kusikiliza. Alipoitambua sauti ya Petro, hakulifungua lango kwa ajili ya furaha, bali alipiga mbio, akaingia ndani, akawaambia kwamba Petro anasimama mbele ya lango. Wakamwambia unawazimu, lakini yeye akakaza sana, akisema kwamba ndiyo hivyo. Wakanena ni malaika wake. Petro akafuliza kugonga hata walipokwisha kumfungulia, wakamwona wakastaajabu. Naye akawapungia mkono wanyamaze akawaeleza jinsi Bwana alivyomtoa katika gereza. Akasema kampasheni Yakobo na wale ndugu wengine habari hizi. Akaondoka akaenda mahali pengine."* (Matendo. 12:5-17)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Yeremia 29:12; 42:3, Mathayo 5:44; 7:11; 2 Nyakati 7:14; Zaburi 32:5-11; 1 Thessalonike 5:17)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO** - Yesu anawafundisha wanafunzi wake kwamba pale unapoomba, BWANA Mungu anakusikia. Yesu anasema tuombe tunapokuwa na hitaji. Wakati mnapoomba miujiza hutokea.

# WEKA AKIBA (HAZINA) YAKO MBINGUNI

SOMO 2-10

*Kumweshimu Mungu kwa Maisha na Mali zetu*

## KIINI CHA SOMO- *Kuandaa udongo*

Wale wote watakaopata thawabu mbinguni itategemea walifanya nini katika kumheshimu Mungu katika maisha na mali zao walipokuwa hapa duniani. Hivyo, wafuasi wanatakiwa kuishi wakiwa na matumaini ya kuwa ziko thawabu tayari kwa ajili yao mbinguni kwa kazi njema walizozifanya hapa duniani.

Andiko Kuu: *"Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekee hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wavi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwepo na moyo wako."(Mat 6:19-21)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Yesu alipata heshima kula chakula cha jioni katika nyumba ya Lazaro. Yesu alikuwa amekwisha mfufua Lazaro kutoka kwa wafu. Wageni akiwemo Lazaro pamoja na dada yake Lazaro aliyeitwa Martha na Maria pamoja na wanafunzi.

**Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-**

"*Basi siku sita kabla ya pasaka, Yesu alifika Bethania, alipokuwapo lazaro, yeye ambaye alimfufua katika wafu. Basi wakamwandalia karamu huko; naye Martha akatumika; na lazaro alikuwa mmoja wao walioketi chakulani pamoja naye. Basi Mariamu akatwaa ratli ya Marhamu ya nardo safi yenye thani nyingi, akampaka Yesu miguu, , akamfuta Yesu miguu kwa nywele zake. Nayo nyumba pia ikajaa harufu ya Marhamu Basi Yuda Iskariote, mmojawapo wa wanafunzi wake ambaye ndiye atakaye kumsaliti akasema, Mbona Marhamu hii haikuuzwa kwa dinari mia tatu, wakapewa maskini? Naye aliyasema hayo si kwa kuwahurumia maskini; bali kwa kuwa ni mwivi, naye ndiye aliyeshika mfuko, akavichukua vilivyotiwa humo. Basi Yesu alisema, mwache aiweke kwa siku ya maziko yangu. Kwa maana maskini mnao siku zote pamoja nanyi; bali mimi hamnami siku zote.*" (Yn. 12:1-8)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Timotheo 6:17-19; Luka 12:32-34; 1 Korintho 3:10-17; Marko 8:34-38)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO** - Yesu atuambia tufanye vitu ambavyo vitatuhesabia umilele. Mungu huwatunuku wote wanaomheshimu kwa uhai na mali zao.

SOMO
2-11

# USIOGOPE

*Mungu anajua na anajali mahitaji yako*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Yesu anasema kuwa anatujali kuhusu maisha yetu, na atatusaidia katika matatizo yetu. Pale tunapokuwa na wasiwasi kuhusu maisha yetu tunakuwa hatuna imani na Yesu.

Andiko la Msingi: *“.....**Basi msisumbukie ya kesho, kwa kuwa kesho itajisumbukia yenyewe. Yatosha kwasiku maovu yake**”* (Mathayo 6:34)

## **Simulizi ya Biblia** -*Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Yesu akiwa pamoja na wanafunzi wake ziwani, wanafunzi wake wengi walikuwa ni wavuvi ziwani

***Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-***

*“Siku ile kulipokuwa jioni, akawaambia na tuvuke mpaka ng'ambo. Wakauacha mkutano , wakamchukuwa vile alivyo katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwapo pamoja naye ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji naye mwenyewe alikuwa katika Shetri, amelala juu ya mto; wakamwamsha wakamwambia, mwalimu si kitu kwako kuwa tunaangamia? Akaamka akaukemea upepo akaiambia Bahari, nyamaza, utulie. Upepo ukakoma kukawa shwari. Akawaambia, mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado? Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, ninani huyu, basi, hata upepo wa bahari wamtii”* (Marko. 4:35-41)

## **MCHAKATO wa UGUNDUZI** - ***Maji na rutubisha***

## **MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA** - *Kupunguza*

*(Mithali 3:5-6; Luka 12:22-25; Ebrania 11:8-12; Galatia 2:20; 1 Petro 1:21)*

## **MAOMBI NA MASWALI/MSINGI** - ***Kuvuna Matunda*** *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO** -Yesu hutujali katika kila nyanja ya maisha yetu. Tunahitaji kuweka imani zetu na kumwamini yeye.

# USIWAHUKUMU WENGINE

*Mungu ni hakimu*

SOMO 2-12

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Ni kinyume kuwahukumu wengine, watu wote ni wenye dhambi na Mungu pekee ndiye anaweza kuhukumu.

Andiko la msingi: ***"Msihukumu msije mkahukumiwa ninyi kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo, ndiyo mtakayohukumiwa; na kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa. Basi mbona wakitazama, kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe, huiangalii?"*** **(Mt 7:1-3)**

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Mafarisayo, Mafarisayo na Waandishi walijua sheria za dini na walitakiwa kuhakikisha kwamba watu wanatii sheria hizi za dini.

***Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-***

*"Hata asubuhi kulipokucha akaingia tena hakaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi, akawa akiwafundisha. Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati. Wakamwambia, mwalimu, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini. Basi katika torati, , Musa alituamuru kuwapiga mawe wanawake namna hii nawe wasemaje, nao walisema neno hili ili wapate kumjaribu, ili wapate sababu ya kumshitaki. Lakini Yesu akainama akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao walipozidi kumhoji alijiinua akawaambia, yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wakumtupia jiwe. Akainama tena akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao waliposikia wakashtakiwa na dhamili zao wakatoka mmoja mmoja, wakianzia tangu wazee na hata wa mwisho wao, akabaki Yesu pekee na Yule mwanamke amesimama katikati. Yesu akajiinua asimwone mtu ila Yule mwanamke. Akamwambia, mwanamke, wako wapi, washtaki wako? Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? Akamwambia hakuna Bwana. Yesu akamwambia wala mimi sikuhukumu. Enenda zako wala usitende dhambi tena"* (Yn 8:2-11)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - ***Maji na rutubisha***

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Yakobo 4:12; Yohana 8:14-18; 1 Korintho 4:3-5; Luka 6:37)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - ***Kuvuna Matunda*** *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO** - Mungu ndiye hakimu wa haki. Watu hawataweza kuhukumu kwa haki.

# OMBENI, TAFUTENI, BISHENI

SOMO 2-13

*Mungu huyakubali maombi ya mtu anayejishusha*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa udongo*

Mungu anatufundisha kwamba tunapoomba, tunapotafuta na kubisha mara kwa mara, Yeye hujibu kwa sababu ya uhusiano wetu na Mungu, tunaweza kuendelea kumtafuta Mungu. Mara nyingine maombi yetu yanaweza yasijibiwe haraka.

Andiko la msingi: ***"Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtaona, bisheni, nanyi mtafunguliwa, kwa maana kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona, naye abishae atafunguliwa."*** **(Mt 7:7-8)**

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda mbegu*

*Utangulizi unatoa maelezo yenye kusaidia kuelewa kwa urahisi sana simulizi za BWANA Yesu Kristo.*

Yesu anawaambia wanafunzi wake kuwa ni lazima waombe kila wakati, pasipo kukata tamaa.

***Simulizi ya Biblia inaanzia hapa:-***

*"Akasema, palikuwa na kadhi katika mji fulani, hamchi mungu na wala hajali watu. Na katika mji huo palikuwa na mwanamke mjane, aliyekuwa akimwendea mwendea, akisema, nipatie haki na adui yangu. Naye kwa muda alikataa; halafu akasema moyoni mwake, ijapokuwa simchi mungu na sijali watu, lakini, kwa kuwa mjane huyu ananiudhi,, nitampatia haki yake, asije akanichosha kwa kunidai daima. Bwana akasema, sikilizeni alivyosema Yule kadhi dhalimu. Na Mungu je! Hatawapatia haki wateule wake waliomlilia mchana na usiku, naye ni mvumilivu kwao? Nawaambia atawapatia haki, upesi; walakini atakapokuja mwana wa Adamu, je! Ataiona imani duniani?"* (Lk 18:2-8)

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*


*(1 Yohana 3:21-22; 5:14-15; Ebrania 4:16; Yakobo 4:2-3; 5:16; Efeso 6:18; Kolosai 4:12)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI - *Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**====HITIMISHO** -Yesu anatufundisha kuwa tuombe kila wakati pasipo kuvunjika moyo. Yesu anatufundisha kuwa tuombe kila wakati pasipo kuvunjika moyo. Tukiwa tunaomba mara kwa mara, Mungu atasikia sauti zetu na atatujibu.

www.iBFAM.org

KUZAA NA KUONGEZEKA



# MAISHA TELE

Mpangilio wa Masomo **3** *Kuta*

*Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kasha wawe nao tele (Yohana 10:10)*

# *Kuta*

## Mpangilio wa Tatu wa Masomo

## *Ukurasa*

**Masomo:**


3-1 Mfuate Kristo....49

Yesu hutuita sisi tumfuate

3-2 Mfuate Kristo....50

Kumfuata Kristo Hutuhitaji Sisi Kuwa na Tumaini na Kumtegemea

3-3 Mfuate Kristo....51

wale wanaomfuata Yesu Kristo huondoka kwa wengine

3-4 Waambiye Wengine Kuhusu Yesu....52

kuwaongoza wengine kumfuata Yesu

3-5 Waambiye Wengine Kuhusu Yesu....53

waambiye habari njema wengine

3-6 Waambiye Wengine Kuhusu Yesu....54

watu wengi wapo tayari kusikiliza habari

3-7 Kumpenda Mungu....55

kuwa na uhusiano na Mungu ni jambo muhimu sana

3-8 Kumpenda Mungu....56

kumfahamu mchungaji mwema

3-9 Kuwapenda Wengine....57

kuishi kwa umoja na wafuasi wengine wa Kristo

3-10 Kuwapenda Wengine....58

Kuwa nuru ya ulimwengu

3-11 Kuwafanya Wanafunzi....59

lisha kondoo zangu

3-12 kuwafanya wanafunzi....60

Yesu yupo pamoja nasi kama tunavyowafanya wanafunzi

3-13 Kuwafanya Wanafunzi.... 61

kuwatia nguvu na kuwatia moyo waamini

# MFUATE KRISTO

*Yesu Hutuita Sisi Tumfuate*

SOMO 3-1

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

yesu huwataka watu wamfuate. Wafuasi wa Kristo ni wale wanaotazama na kumfuata katika njia zake na mafundisho

**Andiko la Msingi**: *Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza, na mtu atakaye kuipoteza, nafsi yake kwaajili yangu ataiona" (Mathayo 16:24-25)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu alipoanza huduma yake ya hadhara, mojawapo ya mambo ya kwanza aliyoyafanya ni kuwaita wanafunzi wake kumfuata yeye na kujifunza njia zake.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Naye alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya, aliona ndugu wawili, Simoni aitwae Petro, na Andrea nduguye, wakitupa jarifa baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. Akawaambia, nifuateni, name nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. Mara wakaziacha nyavu zao wakamfuata. Akaendelea mbele akaona ndugu wengine wawili Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, ambao walikuwako chomboni pamoja na Zebedayo baba yao wakitengeneza nyavu zao, akawaita. Mara wakakiacha chombo na baba yao, wakamfuata. (Mathayo 4:18-22)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Mathayo19:21; Yohana 8:12; Yohana 10:27; Luka 9:57-62)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* (2 Timotheo3:16-17)

**===HITIMISHO** - Yesu hutuuliza sisi kumwagilia kwa makini na kufuata njia zake.

# MFUATE KRISTO

SOMO 3-2

*Kumfuata Kristo Huhitaji Sisi Kuwa na Tumaini na Kumtegemea*

## KIINI CHA SOMO *- Kuandaa Udongo*

Kumfuata Yesu maana yake ni kuweka mategemeo yetu na matumaini yetu katika yeye. Kitu chochote tulichonacho katika maisha yetu tunachokitegemea na kukitumaini, kinaweza kuwa kikwazo kwa utimilifu wa kumfuata Yesu.

**Andiko la Msingi**: *Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza, na mtu atakaye kuipoteza, nafsi yake kwaajili yangu ataiona" (Mathayo 16:24-25)*

## Simulizi ya Biblia *- Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Utajiri ni mojawapo ya mambo ambayo watu wanaweka tegemeo lao, na tumaini lao katika huo.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Natazama mtu mmoja akamwendea akamwambia, mwalimu, nitende jambo gani jema, ili nipate uzima wa milele? Akamwambia kwani kuniuliza habari ya wema? Aliye mwema ni mmoja. Lakini ukitaka kuingia katika uzima zishike amri. Akamwambia zipi? Yesu akasema; ni hizi, usiue, usizini, usiibe, usishuhudiye uongo, waheshimu baba yako na mama yako, mpende jirani yako kama nafsi yako. Yule kijana akamwambia, haya yote nimeyashika; nimepungukiwa na nini tena? Yesu akamwambia, ukitaka kuwa mkamilifu, enenda ukauze ulivyonavyo, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni, kasha njoo unifuate. Yule kijana aliposikia neno lile, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi. (Mathayo 19:16-22)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI *- Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA *- Kupunguza*

*(Mathayo 6:19-21; Mithali 3:5-6; Rumi15:13; 1 Thesalonoke 1:3)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI *-Kuvuna Matunda* (2 Timotheo 3:16-17)

**===HITIMISHO**- Wafuasi wa Kristo wangeliweka tegemeo lao na tumaini lao kwa Kristo peke yake

# MFUATE KRISTO

SOMO 3-3

*Wale Wanaomfuata Yesu Kristo Huondoka kwa Wengine*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu alikuja kutafuta na kuokoa waliopotea. Kuwa mfuasi wa Yesu Kristo maana yake ni kwamba utawafikia waliopotea kama Yesu alivyofanya.

**Andiko la Msingi**: *Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake anifuate. Kwa kuwa mtu atakaye kuiokoa nafsi yake, ataipoteza, na mtu atakaye kuipoteza, nafsi yake kwaajili yangu ataiona" (Mathayo 16:24-25)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu alikuwa akifundisha ukweli kupiatia pande zote za nchi, watu wengi walikuwa wanakuja kusikia maneno ya Yesu, aliyokuwa akifundisha.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*akatoka tena akaenda kando ya Bahari, mkutano wote wakamwendea, akawafundisha. Hata alipokuwa akipita akamwona lawi wa Alfayo, ameketi phorodhani, mwake, watoza ushuru wengi na wenye dhambi waliketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake; kwa maana walikuwa wengi wakimfuata. Na waandishi na mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwaambia wanafunzi wake; mbona anakula na watoza ushuru na wenye dhambi? Yesu aliposikia aliwaambia, wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi" (Marko 2:13-17)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Mithali19:17; Luka15:1-31; Luka 19:10; Galatia6:9-10, Yakobo 3:18)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Kama wafuasi wa Yesu, tutawafikia waliopotea wanaotuzunguka kama Yesu alivyowafikia waliomzunguka

# WAAMBIE WENGINE KUHUSU YESU

SOMO 3-4

*Kuwaongoza Wengine Kumfuata Yesu*

## KIINI CHA SOMO *- Kuandaa Udongo*

Mungu anataka tuwe na mahusiano na watu wote. Kama wafuasi wa Kristo, tumeitwa kuwaongoza wengine kuwa na mahusiano na yeye.

**Andiko la Msingi**: *Basi wamwitaje yeye wasiyemwa? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje pasipo mhubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa? Tena wapelekwaje wasipojitoa? Ni mizuri kama nini miguu yao, wahubirio habari ya mema!" (Rumi10:14-15)*

## Simulizi ya Biblia *- Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi. .*

Simoni Petro alikuwa ni mvuvi kitaaluma kabla hajawa mfuasi wa Yesu. Katika hadithi hii Yesu alimwita Petro kuwa mvuvi wa watu.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Ikawa mkutano walipomsonga wakilisikiliza neno la Mungu, yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa Genezareti, akaona vyombo viwili vimekaa kando ya ziwa, lakini wavuvi wametoka wanaosha nyavu zao. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akamtaka akipeleke mbali kidogo na Pwani. Akaketi akawafundisha makutano ali chomboni. Hata alipokwisha kunena alimwambia Simoni, tweak mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mkavue samaki. Simoni akajibu akamwambia, Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu. Basi walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mkono washiriki wao walikuwa katika chombo cha pili, waje kuwa saidia; wakaja wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama. Simony alipoona hayo alianguka magotini pa Yesu, akisema, ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana. Maana alishikwa na mshangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki waliopata; na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washiriki wa Simoni. Yesu akamwambia Simoni, usiogope, tangu sasa utakuwa ukivua watu. Hata walipokwisha kuviegesha pwani vyombo vyao wakamfuata, wakaacha vyote wakamfuata. (Luka 5:1-11)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI *- Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA *- Kupunguza*

*(Mathayo28:18-19; 2 Petro 3:9; Yohana 4:39-42)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI *-Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Mungu anahitaji kuwa na mahusiano na watu wote. Kama wafuasi wa Kristo tuna faida ya kuwaongoza watu wengine, wawe na uhusiano na watu wengine.

# WAAMBIYE WINGENE KUHUSU YESU

SOMO 3-5

*Waambiye Habari Njema Wengine*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Biblia inawaambia watu washiriki habari njema za Yesu na watu wengine. Watu wote wanastahilikuwa na fursa kusikia habari njema ambazo Bwana Yesu alizileta.

**Andiko la Msingi**: *Basi wamwitaje yeye wasiyemwa? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje pasipo mhubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa? Tena wapelekwaje wasipojitoa? Ni mizuri kama nini miguu yao, wahubirio habari ya mema!" (Rumi 10:14-15)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Paulo alikuwa mwalimu na mhubiri aliyejulikana. Katika hadithi hii, Paulo alihubiri injili. Injili ni habari njema ambazo Mungu huhitaji uhusiano na watu wote. Tunaweza kuwa na uhusiano na mungu kwa sababu Yesu alijitoa sadaka kwaajili ya dhambi zetu.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Paulo akatokewa na maono usiku; alimwona mtu wa makedonia amesimama, akimsihi na kumwambia, vuka, uje makedonia utusaidie. Basi alipokwisha kuyaona yale maono, mara tukataka kutoka kwenda Makedonia, kwa kuwa tuliona hakika kwamba Mungu ametuita kuwahubiri tuwa hubiri habari njema. Basi tukang'oa nanga kutoka troa, tukafika samo Thrake kwa tanga moja, na siku ya pili tukafika Neopoli; na kutoka hapo tukafika filipi, mji wa Makedonia, mji ulio mkuu katika jimbo lile, mahali walipohamia Warumi; tukawa katika mji huu, tukikaa siku kadha wa kadha. Hata siku ya sabato tukatoka nje ya lango, tukaenda kando yam to, ambapo tukadhani ya kuwa pana mahali pa kusali; tukaketi tukisema na wanawake waliokuwa pale. Mwanamke mmoja jina lake Lidia, mwenye kuuza rangi ya zambarao, mwenyeji wa Thiatira, mcha Mungu, akatusikiliza, ambaye moyo wake ulifunguliwa na Bwana, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo. Hata alipokwisha kubatizwa yeye na nyumba yake, akamsihi akisema, kama mmeniona kuwa mwaminifu kwa Bwana, ingieni nyumbani mwangu mkakae, akatushurutisha.. (Matendo 16:9-15)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Mathayo 10:7-8; Mathayo 28:19-20; Marko 16:15; 1 korintho2:1-5; Rumi 1:16-17)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Biblia husema wale wanaomfuata Yesu wameitwa kuwaambia watu wengine habari njema ili kwamba kila mmoja awe na mahusiano binafsi na Mungu.

# WAAMBIYE WENGINE KUHUSU YESU

SOMO 3-6

*Watu Wengi Wapo Tayari Kusikiliza Habari*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu alisema mavuno ni mengi lakini watenda kazi ni wachache. Kuna watu wengi wanasubiri kusikia kuhusu Yesu Kristo. Wafuasi wa Kristo watashiriki habari njema pamoja na watu wote.
.

**Andiko la Msingi**: *Basi wamwitaje yeye wasiyemwa? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje pasipo mhubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa? Tena wapelekwaje wasipojitoa? Ni mizuri kama nini miguu yao, wahubirio habari ya mema!" (Rumi 10:14-15)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu aliwapa maelekezo wanafunzi wake jinsi ya kushiriki na wengine habari njema

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Basi baada ya hayo, Bwana aliweka na wengine, sabini, akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe. Akawaambia, mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apelike watenda kazi katika mavuno yake. Enendeni, angalieni, nawatuma kama wanakondoo kati ya mbwa mwitu. Msichukue mfuko, wala koba, wala viatu, wala msimwamkie mtu njiani. Na nyumba yoyote mtakayoingia semeni kwanza, amani iwemo nyumbani humu; na akiwamo mwana wa amani yenu itamkalia; la hayumo amani yenu itarudi kwenu. Basi kaeni katika nyumba iyo hiyo, mkila na kunywa vya kwao; maana mtenda kazi amestahili kupewa ujira wake. Msihame, hame kutoka nyumba hii kwenda nyumba hii. Na mji wowote mtakaouingia, wakiwakaribisha, vileni vyakula viwekwavyo mbele yenu; waponyeni wagonjwa waliomo, waambieni, ufalme wa Mungu umekaribia" (Luka 10:1-9)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Mathayo 9:35-38; Yohana 4:35-38; Isaya 6:8; Galatia 6:9-10)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* (2 Timotheo 3:16-17)

**===HITIMISHO**- Tumeainishwa na habari njema za injili. Tuna faida ya kushiriki habari njema na walimwengu wanaotuzunguka.

# KUMPENDA MUNGU

SOMO 3-7

*Kuwa na Uhusiano na Mungu ni Jambo Muhimu Sana*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu aliwauliza wanafunzi wake kufanya mambo mengi. Jambo lililomuhimu zaidi ni mahusiano na Mungu.

**Andiko la Msingi**: *Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote. (Marko 12:30)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Mariamu na Martha walikuwa wafuasi wa Yesu, na walikuwa na mahusianoa mazuri naye.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Ikawa katika kuenenda kwao, aliingia katika kijiji kimoja; mwanamke mmoja jina lake Martha, akamkaribisha nyumbani mwake. Naye alikuwa na umbu lake aitwae Mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesuakasikiliza maneno yake. Lakini Martha alikuwa akihangaika kwa utumishi mwingi; akamwendea akasema; Bwana, huoni vibaya ndugu yangu huyu alivyoniacha nitumike peke yangu? Basi mwambie anisaidie. Bwana akajibu akamwambia, Martha, Martha, unasumbuka na kufadhaika kwaajili ya vitu vingi; lakini kinatakiwa kitu kimoja tu, na Mariamu amelichagua fungu lililojema, ambalo halitaondolewa" (Luka 10:38-42)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Yohana14:15; Mathayo 11:28-30; Filipi 2:12-13; Luka6:47-49)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* (2 Timotheo 3:16-17)

**===HITIMISHO**- Amri iliyo muhimu sana iliyotolewa na Bwana Yesu ni kwamba tumpende yeye kwa moyo wetu, wote, nafsi, akili na nguvu.

# KUMPENDA MUNGU

SOMO 3-8

*Kumfahamu Mchungaji Mwema*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Wafuasi wa Kristo wanatakiwa kumpenda Mungu pamoja na kila sehemu kama jinsi walivyo. Kumpenda Mungu pamoja na vyote walivyonavyo. Na lazima tutamjua Mungu.

**Andiko la Msingi**: *Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote.. (Marko 12:30)*

## Simulizi ya Biblia -*Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu alishaeleza kabla kwamba wafuasi wake, ni kama kondoo, na kondoo humfuata mchungaji.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Basi Yesu aliwaambia tena, Amin, Amin, nawaambia, mimi ndimi mlango wa kondoo. Wote walionitangulia ni wevi na wanyang'anyi. Lakini kondoo hawakuwasikia. Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi ataokoka; ataingia, ataingia na kutoka, naye atapata malisho. Mwivi haji ila aibe, na kuchinja, na kuharibu, mimi nalikuja ili wawe na uzima, kasha wawe nao tele. Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema hutoa uhai wake kwaajili ya kondoo. Mtu wa mshahara wala si mchungaji, ambaye kondoo si mali yake, humwona mbwa mwitu anakuja, akawaacaha kondoo na kukimbia kwa kuwa ni mtu wa mshahara, wara mambo ya kondoo si kitu kwake. Mimi ndimi mchungaji mwema, nami waliowangu nawajua, nao walio wangu wanijua mimi;" (Yohana 10:7-14)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Zaburi23; Zaburi100; Mathayo 9:35-36)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Tukimjua Mungu, tutampenda Mungu

# KUWAPENDA WENGINE

SOMO 3-9

*Kuishi Kwa Umoja na Wafuasi Wengine wa Kristo*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Wafuasi wa Kristo wanaitwa kanisa. Mungu anatazamia kanisa kuishi kwa umoja.

**Andiko la Msingi**: *mpende jirani yako kama nafsi yako. (Marko 12:31)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Viongozi wa dini waliompinga Yesu waliwaambia viongozi wa kanisa, wasizungumze au kufundisha kuhusu Yesu. Kanisa lilimtafuta Mungu kwa mwitikio mzuri.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-.***

*"Basi sasa Bwana yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena neno kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la mtumishi wako mtakatifu yesu. Hata walipokwisha kumuomba Mungu mahali pale walipokwisha kukusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu, kwa ujasiri. Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na Roho moja; na wala hakuna mmoja aliyesema, kitu chochote alichonacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika. Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa Nguvu nyingi na neema nyingi ikawa juu yao wote. Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu ya watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaleta thamani ya vitu vile vilivyouzwa". (Matendo 4:29-35)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Korintho 12:12-31; 1 Korintho 14:26; Efeso 4:1-16; Rumi 12:3-21)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Tumeitwa kuishi kwa umoja pamoja na wafuasi wengine wa Kristo

# KUPENDA WENGINE

*Kuwa Nuru ya Ulimwengu*

SOMO 3-10

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuwapenda watu. Wakristo wameitwa kupeleka ujumbe na matumaini na amani kwa ulimwengu. Wakristo wamefundishwa kuonyesha upendo wa Mungu kwa wale walio katika uhitaji.

**Andiko la Msingi**: *Mpende jirani yako kama nafsi yako (Marko 12:31)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Biblia hutufundisha sisi kuwapenda majirani zetu. Mwanadini stadi alimuuliza Yesu jirani yangu ni nani. Yesu aliitikia kwa mfano wa kuhani, mlawi na msamaria. Walawi na makuhani walikuwa ni watu wa dini sana. Wasamaria walikuwa ni kundi la watu ambao hawakuwa marafiki na kundi ambalo Yesu alikuwa anahusika nalo.

.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***.

*Yesu akajibu akasema, mtu mmoja alishuka toka Yelusalemu kwenda Yeriko, akaangukia kati ya wanyang'anyi wakamvua Nguo ,walimtia jeraha, wakaenda zao, wakamwacha karibu na kufa. Kwa nasibu kuhani mmoja alishuka kwa njia ile. Na alipomwona alipita kando. Na mlawi vivyo hivyo alipofika pale akamwona akapita kando. Lakini msamaria mmoja katika kusafiri kwake alifika pale alipo; na alipomwona alimhurumia akamkaribia, akafunga jeraha, akamtia mafuta na divai; akampandisha juu ya mnyama wake, akampeleka mpaka nyumba ya wageni, akamtunza. Hata siku ya pili akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akisema mtunze huyu, na chochote atakacho gharimiwa zaidi mimi nitakaporudi nitakulipa. Waonaje wewe katika hao watatu, ni yupi aliyekuwa jirani yake Yule aliyeangukia kati ya wanyang'anyi? Akasema ni huyo aliyemwonea huruma. Yesu akamwambia, enenda zako nawe ufanye vivyo hivyo." (Luka 10:30-37)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Yohana3:16-18; 1 Yohana 4:7-12; Yohana13:34-35; Mathayo 5:14-16; Efeso4:1-3; 1 Korintho 13)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Tunavyowajali wale walio katika uhitaji, tunaonyesha kwa matendo upendo wa Mungu kwa kuwajali watu wengine.

# KUWAFANYA WANAFUNZI

*Lisha Kondoo Zangu*

SOMO 3-11

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Upendo wa Mungu hutuvuta kufunza na kuwajali waamini wengine.

**Andiko la Msingi**: *lichungeni kundi la Mungu lililokwenu, na kulisimamia sisi kwa kulazimishwa bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo (1 Petro5:2)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu alikuwa amesuribiwa na kufufuka kutoka kwa wafu. Asubuhi moja na mapema Yesu alikuta wanafunzi wake, wanavua samaki.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-.***

*Yesu akawaambia njooni mfungue. Wala hakuna mtu katika wale wanafunzi alithubutu kumuuliza u nani wewe? Wakajua ya kuwa ni Bwana. Yesu akaenda akautwaa mkate akawapa, na samaki vivyo hivyo. Hiyo ndiyo mara ya tatu Yesu kuonekana na wanafunzi wake baada ya kufufuka katika wafu. Basi walipokwisha kula Yesu akamwambia, Simoni Petro, Je! Simoni wa Yohana wewe unanipenda kuliko hawa? Akamwambia naam Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda. Akamwambia lisha wana - kondoo wangu akamwambia tena mara ya pili Simoni wa Yohana wanipenda? Akamwambia naam Bwana, wewe wajua kuwa nakupenda, akamwambia chunga kondoo zangu. Akamwambia mara ya tatu Simoni wa Yohana wanipenda? Petro alihuzunika kwa vile alivyomwambia mara ya tatu wanipenda? Akamwambia Bwana wewe wajua yote; wewe umetambua ya kuwa nakupenda. Yesu akamwambia lisha kondoo zangu." (Yohana 21:12-17)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Thesalonike 5:11; Mathayo 28:19-20; 2 Timotheo 2:2; 2 Timotheo 4:2-5; Matendo 20:28; 1 Korintho 9:16-18)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Yesu aliwaambia wafuasi wake, kuwafanya wanafunzi. Kuwafanya wanafunzi maana yake kuwasaidia (kuwatengeneza) na kuwafundisha waamini ili wapate kukua kati mahusiano yao na Mungu.

# KUWAFANYA WANAFUNZI

SOMO 3-12

*Yesu Yupo Pamoja Nasi Kama Tunavyowafanya Wanafunzi*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu anawapenda sana watu wote ndiyo maana aliwauliza wafuasi wake kuwafanya wanafunzi. Yesu aliwaahidi waamini kwamba angekuwa pamoja nao vile wanavyowafanya watu kuwa wanafunzi.

**Andiko la Msingi**: *lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na wala si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo, si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo (1 Petro 5:2)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Yesu alisulibiwa na kuwekwa kaburini siku tatu. Wanafunzi walijifunza kuwa kaburi alimokuwa amewekwa Yesu sasa li wazi.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***.

*Na wale wanafunzi kumi na mojawakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu. Nao walipomwona, walimsujudia, walimsujudia; lakini baadhi yao waliona shaka. Yesu akaja kwao, akasema nao akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la mwana, na la Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:16-20)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Yohana 14:15-17; Ebrania13:5-6; 2 Timotheo2:2; Matendo2:42-47)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwenda na kuwafanya wanafunzi. Wafuasi wa Kristo wameitwa kufundisha waamini wapya ili kwamba waweze kukua katika maarifa yao na imani katika Kristo.

# KUWAFANYA WANAFUNZI

*Kuwatia Nguvu na Kuwatia Moyo Waamini*

SOMO 3-13

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Kama waamini wote tunahitaji kutiwa moyo na kutiwa nguvu katika imani yetu.kama sehemu ya familia ya Mungu, tunahitaji kutunzwa na kutiana moyo kwa kila mmoja wetu.

**Andiko la Msingi**: *kundi la Mungu lililokwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. (1 Petro 5:2)*

## Simulizi ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

*Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.*

Paulo na Barnaba walikuwa wanakwenda kutoka mji hata mji kushirikishana kuhusu Yesu.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-.***

*lakini wanafunzi walipokuwa wakimzunguka pande zote, akasimama akaingia ndani ya mji; na siku ya pili yake akatoka, akaenda zake pamoja na Barnaba mpaka Derbe. Hata walipokwisha kuihubiri injili katika mji ule, na kupata wanafunzi wengi, wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antioki, wakifanya imara Roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile imani nay a kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi. Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kwamba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini (Matendo 14:20-23)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Matendo 18:23; 1 Thesalonike 5:13-15; Matendo 2:42-47; Matendo11:25-30; Matendo 15:30-41)*


## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Ili tuwe wafuasi waaminifu wa Kristo tunahitajika kuwatia nguvu na kuwatia moyo.

iBFAM

www.iBFAM.org

KUZAA NA KUONGEZEKA



# UKWELI ULIO MUHIMU SANA

Mpangilio wa Masomo **4** *Paa*

*"Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"* (Yohana 8:32)

# *Paa*
## Mpangilio wa Nne wa Somo: *Ukurasa*

---

**Masomo:**


4-1 Mungu....................................................64
kuna Mungu mmoja tu.
4-2 Yesu....................................................65
Yesu ni mwana wa Mungu
4-3 Roho Mtakatifu....................................................66
wafuasi wakristo wanamhitaji Roho Mtakatifu
4-4 Upendo na Msamaha....................................................67
Yesu wlikuja kuonyesha upendo na msamaha
4-5 Kuhesabiwa Haki na Mungu....................................................68
kugundua kwamba tumepungukiwa na utukufu wa Mungu
4-6 Ufalme wa Mungu....................................................69
kuwa wa kiroho aliyezaliwa mara ya pili
4-7 Biblia....................................................70
ukweli ulioandikwa kutoka kwa Mungu
4-8 Kanisa....................................................71
wafuasi wa Kristo kuishi kwa pamoja
4-9 Nuru ya Ulimwengu....................................................72
kuangaziwa na nuru ya Kristo
4-10 Umilele....................................................73
kuwa na Mungu milele au kuwa katika mateso ya milele
4-11 Hukumu....................................................74
Yesu Kristo atahukumu watu wote
4-12 Meza ya Bwana....................................................75
umuhimu wa kukumbuka kifo cha Yesu Kristo kwaajili ya dhambi zetu
4-13 Ubatizo....................................................76
Kutangaza mbele za watu juu ya imani ya Kristo

# MUNGU

*Kuna Mungu*
*Mmoja tu.*

SOMO
4-1

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Kuna Mungu mmoja tu. Tunaweza kufahamu Mungu ni nani kupitia Biblia na anafananaje.. biblia huelezea kuwa Wakristo waabudu mungu mmoja tu na kuabudu miungu mingine ni kutotii (kuasi) Mungu mmoja wa kweli.

Andiko la msingi :*Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja . (Marko 12:29)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Paulo alikuwa ni mmoja wa wahubiri wakubwa wa injili. Siku moja Paulo alihubiri ujumbe kuwa julisha watu Mungu mmoja tu wa kweli. Watu wa mji walikusanyika kumsikia Paulo alichokuwa akisema.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Paulo akasimama katikati ya Areapago, akasema, enyi watu wa Athene katika mambo yote naona ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini. Kwa sababu nilipokuwa nikipita huko na huko na kuyaona mambo ya ibada yenu, niliona madhabahu iliyoandikwa maneno haya*, KWA MUNGU ASIYEJULIKANA. *Basi mimi nawahubiria habari zake yeye ambaye ninyi mnamwabudu bila kumjua. Mungu alifanya ulimwengu na vyote vilivyomo, yeye kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono. Wala hatumikiwi kwa mikono ya wanadamu kana kwamba anahitaji kitu chochote. Kwa maana ndiye anayewapo wote uzima na pumzi na vitu vyote. Naye alifanya kila taifa la wanadamu kutoka katika mmoja, wakae juu ya uso wa nchi yote, akiisha kuwawekea nyakati alizoziamuru tangu zamani na mipaka ya makazi yao, ili wamfuate Mungu, ingawa ni kwa kupapasa papasa, wakamwone ijapokuwa hawi mbali na kila mmoja wetu. Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda,na kuwa na uhai wetu. Kamavile mmoja wenu mtunga mashairi alivyosema, maana sisi sote tu wazao wake. Basi kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, hatupasi kudhani ya kuwa Mungu ni mfano wa dhahabu, au fedha au jiwe vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu. Basi zamani zile. Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni. Bali sasa anawaagiza watu wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku ambayo atawahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu Yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote, uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua kutoka katika wafu." (Matendo 17:22-31)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Kumbu kumbu la Torati 6:4-5; 1 Timotheo 2:5-6; Mwanzo1:1; Ufunuo 1:8; Marko 12:32)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- kuna Mungu mmoja tu wa kweli - lazima tuwe na uhakika tusiabudu miungu yoyote ya uongo.

# YESU

*Yesu ni*
*Mwana wa Mungu*

SOMO
4-2

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu alikuwa mbinguni na Mungu, kabla hajaja duniani. Yesu ni mwana pekee wa Mungu. Baada ya kifo chake na ufufuo kutoka kwa wafu, Yesu alirudi kwa baba yake mbinguni. Kumfahamu na kumwabudu Yesu ndiyo njia ambayo tungelipaswa, ni lazima tujue Mungu Baba na Yesu ni mmoja.

Andiko la msingi: *haya yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa mana: " Bii" (Yaani "Mungu yupo pamoja nasi"). (Mathayo 1:22-23)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Kwa kupitia historia kulikuwa na watu wengi waliopelekwa na Mungu kutangaza kuwa ipo siku moja Yesu angelikuja.watu hawa waliitwa manabii: Musa na Eliya ni manabii walioishi miaka mingi kabla ya kuja kwa yesu duniani.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Na baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye akawaleta juu yam lima mrefu faraghani, akageuka sura yake mbele yao uso wake ukang'aa kama jua, mavazi yake yakawa meupe kama nuru. Na tazama wakatokewa na Musa na Eliya wakizungumza naye. Petro akajibu akamwambia Yesu, Bwana ni vizuri sisi kuwapo hapa, ukitaka nitafanya hapa vibanda, kimoja chako wewe, na kimoja cha Musa, na kimoja cha Eliya. Alipokuwa katika kusema natazama wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye, msikieni yeye. Na wale wanafunzi waliposikia walianguka kifulifuli, wakaogopa sana. Yesu akaja akawagusa akasema inukeni wala msiogope. Wakainua macho wasione mtu ila Yesu peke yake (Mathayo 17:1-8)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Ebrania1:1-3; Yohana 1:1-5; Korintho 1:15-20; Korintho 2:9; Filipi 2:5-11; Yohana 3:16)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* (2 Timotheo 3:16-17)

**===HITIMISHO** - Mungu na Baba mbinguni ni mmoja - Yesu ni Mungu

# ROHO MTAKATIFU

SOMO 4-3

*Wafuasi Wakristo Wanamhitaji Roho Mtakatifu*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuwa uhusiano na Roho mtakatifu ni wa muhimu sana. Yesu alikuwa na uhusiano na Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu anaitwa msaidizi na atawaongoza wafuasi wa Kristo kwenye kweli. Roho Mtakatifu huwapa pia wafuasi nguvu ya Kristo. Kwa waamini wa leo haya mahusiano ya ki-Mungu yanaendelea kuwa muhimu.

Andiko la msingi: ***□ami ni□am□ □mba Baba□nay□ a□a□apa m□ai□izi m□in□in□□ili a□a□ nanyi ha□a □n□iy□ □□h□ □a □□□li ambay□ ulim□ □n□u hau□ □zi □ump□□□a□□□a □u□a haum□ □ni □ala ham□ambui□ bali ninyi mnam□ambua□maana ana□aa □□ □nu nay□ a□a□u□a n□ani y□nu*** *(Yohana 14:16-17)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Moja wapo ya maelekezo ya mwisho ya Yesu aliyowapa wafuasi wake, ilikuwa ni kumsubiri Roho Mtakatifu. Katika kutii kundi kubwa la watu walikusanyika Yelusalemu kumsubiri. Baada ya siku si nyingi alikuja juu yao wale waliokusanyika.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Hata ilipotimia siku ya pentecoste, walikuwapo watu mahali pamoja, kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana , kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine kama Roho alivyowajalia kutamka.*

*Na walikuwako Yelusalemu wayahudi wakikaa, watu wataua watu wa kila taifa chini ya mbingu. Basi sauti ilipofikiwa makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe. Wakashangaa wote wakastaajabu, wakiambiana, tazama hawa wote wasemao si wagalilaya? Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu aliyozaliwa nayo? Waparthi, na Wamedi na waelami, nao wakaao mesopotania, uyahudi na kapadokia, na Pento na Asia, Frigia na Pamfilia Misri na pande za Libia karibu na Krene na wageni watokao Rumi. Wayahudi na waongofu, Wakrete na Warabu; tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu matendo makuu ya Mungu, wakashangaa wote wakaingiwa na shaka wakiambiana, maana yake ni nini mambo haya? Wengine walidhihaki wakisema, wamelewa kwa mvinyo mpya.*

*Lakini Petro alisimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake akawaambia, Enyi watu wa uyahudi na ninyi nyote mkaao Yelusaremu, lijueni jambo hili mkasikilize maneno yangu. Sivyo mnavyodhani, watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lile lililonenwa na kinywa cha nabii Yoeli. Itakuwa siku za mwisho asema Bwana Mungu nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona ." (Mdo 2:1-17)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Yohana 16:13; Matendo 1:8; Luka 11:13; 1 Korintho 12:7-11; Galatia 5:16; Galatia 22-23)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* (2 Timotheo 3:16-17)

**===HITIMISHO** - Wafuasi wa kwanza wa Yesu walikuwa na nguvu ya kubadirisha ulimwengu waliouishi kwa sababu walikuwa wamejazwa na Roho Mtakatifu. Leo kama wafuasi wa kwanza wa Kristo tunamhitaji Roho Mtakatifu.

# UPENDO NA MSAMAHA

SOMO 4-4

*Yesu Alikuja Kuonyesha Upendo na Msamaha*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu alionyesha upendo na msamaha kwa watu wote. Kama wafuasi wa Kristo tungelipaswa pia kuonyesha upendo wa msamaha wa Mungu kwa watu.

Andiko la msingi: *Amri yangu ni hii, mpendane kama nilivyowapenda ninyi (Yohana 15:12)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Wakati Yesu alipoishi, watu walikuwa wanatawaliwa na sheria ya Musa, katika hadithi hii, Yesu anawaonyesha watu njia mpya ya kuishi, ambayo iko kwenye msingi wa upendo na msamaha

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*hata asubuhi kulipokucha akaingia tena hakaluni, na watu wote wakamwendea; naye akaketi, akawa akiwafundisha. Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati. Wakamwambia, mwalimu, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini. Basi katika torati, , Musa alituamuru kuwapiga mawe wanawake namna hii nawe wasemaje, nao walisema neno hili ili wapate kumjaribu, ili wapate sababu ya kumshitaki. Lakini Yesu akainama akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao walipozidi kumhoji alijiinua akawaambia, yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wakumtupia jiwe. Akainama tena akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao waliposikia wakashtakiwa na dhamili zao wakatoka mmoja mmoja, wakianzia tangu wazee na hata wa mwisho wao, akabaki Yesu pekee na Yule mwanamke amesimama katikati. Yesu akajiinua asimwone mtu ila Yule mwanamke. Akamwambia, mwanamke, wako wapi, washtaki wako? Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia? Akamwambia hakuna Bwana. Yesu akamwambia wala mimi sikuhukumu. Enenda zako wala usitende dhambi tena." (Yohana 8:2-11)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Yohana 2:8-11; 1 Yohana3:16; 1 Yohana 4; Yohana 15:12-17)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** - Yesu alikuwa mkamilifu wa kuonyesha kwa matendo, upendo, na msamaha kama sisi, ni wafuasi wa Kristo tungelipaswa kuonyesha kwa matendo, upendo na msamaha kwa watu wote.

# KUHESABIWA HAKI NA MUNGU

SOMO 4-5

*Kugundua KwambaTumepungukiwa na Utukufu Wa Mungu*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Watu wote wamepungukiwa na utukufu wa Mungu. Hatuwezi kujifanya wema sisi wenyewe kwa kufanya mambo mazuri. Ni lazima tugundue hali yetu ya dhambi na kumwomba Mungu rehema. Tunapoomba rehema kutoka kwa Mungu ndipo tutakapokuwa tumehesabiwa haki na Mungu.

Andiko la msingi: *Wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.... (Rumi 3:23)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Yesu alieleza hadithi kuhusu watu wawili. Mtu mmoja alikuwa ni kiongozi wa dini, aliyeitwa Falisayo. Mtu mwingine alikuwa mtoza ushuru aliyekuwa amechukiwa na jamii. Katika hadithi hii, kuhesabiwa haki na Mungu maana yake ni kwamba, Mungu alisamehe dhambi ya mtu.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*“Watu wawili walipanda kwenda hekaluni kusali, mmoja falisayo, wa pili mtoza ushuru. Yule falisayo akasimama akiomba hivi moyoni mwake; Ee Mungu nakushukuru kwa kuwa mi si kama watu wengine, wanyang'anyi, wadhalimu, wazinzi, wala wala kama huyu mtoza ushuru. Mimi nafunga mara mbili kwa juma, hutoa zaka katika mapato yangu yote. Lakini Yule mtoza ushuru alisimama mbali wala hakuthubutu hata kuinua macho yake mbinguni, bali alijipigapiga kifua chake akisema; Ee Mungu uniwie radhi mimi mwenye dhambi. Nawaambia huyu alishuka kwenda nyumbani mwake amehesabiwa haki kuliko Yule, kwa maana kila ajikwezae atadhiliwa na kila ajidhiliye atakwezwa” (Luka 18:10-14)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Rumi 3:24; Rumi 4:4-5; Rumi 4:25; Rumi 5:1-2; Rumi 5:8-10; Rumi 10:10; Yakobo 2:20-26)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* (2 Timotheo 3:16-17)

**===HITIMISHO** - Watu wote ni wenye dhambi na wanahitaji kuhesabiwa haki.
Kuhesabiwa haki kunaanza pale tunapogundua kwamba tumepungukiwa na utukufu wa Mungu halafu tuombe rehema kwa Mungu. Mungu peke yake anaweza kutuhesabia haki.

# UFALME WA MUNGU

SOMO 4-6

*Kuwa wa Kiroho Aliyezaliwa Mara ya Pili*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu mara nyingi alizungumza juu ya ufalme wa Mungu. Ufalme wa Mungu ni serikali ya Mungu. Wafuasi wa Kristo ni raia wa Mungu. Hakuna mtu atakayeuona ufalma wa Mungu bila kuzaliwa mara ya pili (kuokoka)

Andiko la msingi: *Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa ni kiumbe kipya; ya kale yamepita; tazama yamekuwa mapya na roho zilizotakaswa!" (2 Korintho 5:17)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Mtu aliyeitwa nikodemu alikuja kwa yesu kumuuliza swali. Nikodemu alikuwa ni kiongozi muhimu wa dini.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*"Basi palikuwa na mtu, mmoja wa Mafarisayo, jiana lake nikodemu, mkuu wa wayahudi. Huyu alimjia usiku akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu umetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe. Isipokuwa Mungu yu pamoja naye. Yesu akajibu akamwambia amini, amini nakuambia mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufalma wa Mungu. Nikodemu akamwambia, awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu, amini, amini nakuambia mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho hawezi kuingia ufalme wa wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, na kilichozaliwa kwa roho ni roho. Usistaajabu kwa kuwa nilikwambia hamna budi kuzaliwa mara ya pili. Upepo huvuma upendako na sauti yake wasikia lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake mtu aliyezaliwa kwa Roho." (Yohana 3:1-8)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Petro1:23; Rumi 6:4; Matendo 1:3; Yohana 18:36; 2 Timotheo 4:18; 2 Petro1:11)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** - Yesu alisema, hakuna mtu atakayeweza kuingia katika ufalme wa Mungu bila ya kuzaliwa mara ya pili. Yesu alimwambia nikodemu kwamba ni lazima azaliwe kwa maji na kwa Roho.

SOMO
4-7

# BIBLIA

*Ukweli Ulioandikwa Kutoka Kwa Mungu*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

**Biblia ni neno la Mungu** takatifu na lina nguvu. Ukweli uliokwenye Biblia unaweza kubadirisha mioyo yetu na akili zetu. Biblia ni ya muhimu sana na ni kitabu kinachotuelezea sisi kwamba Mungu ni nani. Biblia ni katabu cha kipekee ambacho kilikuja kutoka kwa Mungu.

Andiko la msingi: *kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu, makosa yao na kwa kuwaongoza na kuwaadibisha katika haki .ili mtu wa Mungu awe kamili,amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.” (2Timotheo. 3:16 - 17*)

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Kabla ya Yesu kuanza huduma yake mbele za watu, alipambana na shetani, katika mapambano haya, Yesu alisimamia maandiko ili kumshinda shetani.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*kasha Yesu alipandishwa na Roho nyikani , ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, ukiwa ndiwe mwana wa Mungu amuru kwamba mawe haya yawe mkate, naye akajibu akasema, mtu hataishi kwamkate tu, bali kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kasha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamuweka juu ya kinara cha hekalu,akamwambia, ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, jitupe chini, kwa maana imeandikwa, atakuagizia malaika zake, na mikononi mwao watakuchukua usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe. Yesu akamwambia, tena imeandikwa, usimjaribu Bwana Mungu wako. Kasha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno akamwonyesha milki zote za ulimwengu na fahari yake. Akamwambia haya yote nitakupa ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia nenda zako shetani kwa maana imeandikwa, msujudiye Bwana Mungu wako umwabudu yeye peke yake. Kasha Ibilisi akamwacha na tazama wakaja malaika wakamtumikia (Mathayo 4:1-11)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Rumi10:17; Efeso 6:13-17; 2 Petro 1:20-21; Zaburi 119; Yakobo 1:21)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** - Yesu alichagua kupambana na shetani kwa maandiko. Tunaweza pia kutumia maandiko kama silaha ya kuweza kumshinda adui na kama chombo cha kujenga imani yetu.

SOMO 4-8

# KANISA

*Wafuasi wa Kristo Kuishi Kwa Pamoja*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu alipoondoka duniani kurudi kwa Baba yake mbinguni,aliliacha kanisa kama mwakilishi wake wa ulimwengu. Kama wafuasi wa Kristo, tunatakiwa tuishi maisha ya imani (au makubaliano) na wafuasi wengine wa Kristo tutiane moyo sisi kwa sisi katika imani. Kanisa ni mwili wa Kristo, na Yesu ni kichwa cha kanisa.

Andiko la msingi: "*Nami nakuambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.*" *(Mathayo 16:18)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Baada ya Yesu kurudi kwa Baba mbinguni, Roho Mtakatifu alikuja, na idadi ya waamini iliongezeka ghafla. Wakati huo waamini walikuwa wanakutana pamoja kuabudu na kujifunza maandiko pamoja. Waamini hawa walikuwa wanawajali wale waliokuwa katika uhitaji na kuwajali wajane. Kundi la kanisa la kwanza Yelusalemu liliundwa na makundi mawili tofauti. Kundi la kwanza la kanisa lilizungumza kiyunani. Kundi linguine lilizungumza kiebrania. Liliitwa Waebrania wa kiyahudi.makuhani katika hadithi hii ni makuhani wa Kiyahudi.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*"Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung'uniko ya wayahudi wa kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahaulika katika huduma ya kila siku. Wale thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, haipendezi sisi kuliacha neno la mungu na kuhudhuria mezani. Basi ndugu chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho na Hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili. Na sisi tutahudumu katika kuomba na kulihudumia lile neno. Neno hili likapendeza machoni pa machoni pa mkutano wote. Wakamchagua stephano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Philipo, na Prokoro, na Nikamori, na Timoni, na Parnena, na Nikolao mwongofu wa Antiokia; ambao wakawaweka mbele ya mitume, na walipokwisha kuomba, wakaweka mikono juu yao. Neno la Mungu likaenea na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalemu; jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile imani". (Matendo 6:1-7)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Matendo 2:42-47; 1 Korintho 12:12-28; Ebrania 10:25; Waefeso 2:19-21; Waefeso 4:14-16)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** - Biblia inalifananisha kanisa na mwili wa mwanadamu. Katika mwili wa mwanadamu kila sehemu ya mwili inakazi ya kipekee. Na kila sehemu ya mwili hutegemea sehemu zingine. Wafuasi wa Kristo wangalitakiwa kuwa waaminifu kwa majukumu yao na kushiriki kwa kanisa zima.

# NURU
# YA ULIMWENGU

*Kuangaziwa na Nuru ya Kristo*

SOMO
4-9

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Kama wafuasi wa Kristo, maisha yetu yangelitakiwa kuwa mwangaza wa tabia ya Kristo. Tungelitakiwa kuonyesha kwa vitendo ulimwengu Kristo ni nani vile ambavyo tunaishi.

Andiko la msingi: *Vivyo hivyo, nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Makutano ya watu, walimkusanyikia yesu, kusikia mafundisho ya Yesu.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

"*Heli ninyi watakapowashutumu na kuwaudhi na kuwa nenea kila neno baya kwa uongo kwaajili yangu furahini na kushangilia kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni; kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu. Ninyi ni chumvi ya dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu yam lima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo ya waangaza wote waliomo nyumbani". (Mathayo 5:11-16)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Yohana1:7; 1 Yohana2:10; 2 Korintho 4:6; Mathayo 5-7)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO**- Yesu aliwafundisha wafuasi wake jinsi ya kuishi maisha ya tabia njema na pamoja na kazi njema.

# UMILELE

*Kuwa na Mungu Milele*
*Kuwa Katika Mateso ya Milele*

SOMO
4-10

## KIINI CHA SOMO *- Kuandaa Udongo*

Maisha hayaishii pale tunapokuwa tumekufa. Tutaendelea kuishi milele. Watu wote watatoa hesabu kwa maisha walioishi duniani. Wafuasi wa Kristo watakuwa paoja naye milele. Wale ambao hawakumfuata Yesu watashiriki mateso mbali kutoka katika uwepo wa Mungu.

Andiko la msingi: *Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja ambayo watu wote waliomo makabulini, watasikia sauti yake. Nao watatoka wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima. Na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu (Yohana 5:28-29)*

## Simulizi Ya Biblia *- Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Yesu aliwafundisha wafuasi wake kuhusu umilele kwa kutumia hadithi kuhusu tajiri na maskini.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*“Akasema, palikuwa na mtu mmoja tajiri, aliyevaa nguo za rangi ya zambarau, na kitani safi, na kula siku zote kwa anasa. Na maskini mmoja jina lake Lazaro, huwekwa mlangoni pake, ana vidonda vingi, naye alikuwa akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika meza ya Yule tajiri; hata mbwa wakaja wakamlamba vidonda vyake. Ikawa Yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa akazikwa. Basi kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na Lazaro kifuani mwake. Akalia akasema Ee baba Ibrahimu, nihurumie umtume Lazaro, achovye ncha ya kidole chake mjini, auburudishe ulimi wangu, kwa sababu ninateswa katika moto huu. Ibrahimu akasema; mwanangu, kumbuka ya kwamba wewe uliyapokea mambo mema yako katika maisha yako, na Lazaro vivyo alipata mabaya, na sasa yeye yupo hapa anafarijiwa, na wewe unaumizwa, na zaidi ya hayo katiyetu sisi na ninyi kumewekwa shimo kubwa. Ili wale watakao kutoka huku kwenda huko wasiweze, na wala watu wa kwenu wasivuke kuja kwetu. Akasema Basi baba nakuomba, umtume nyumbani kwa baba yangu, kwa kuwa ninao ndugu watano, ili awashuhudiye wasije wao pia wakafika mahali hapa pa mateso. Ibrahimu akasema, wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao. Akasema la baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa wafu watatubu. Akamwambia wasipowasikia Musa na manabii, hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu”.(Luka 16:19-31)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI *- Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA *-Kupunguza*

*(1 Thessalonike 4:13-18; Rumi 6:20-23; Mathayo 19:16-26; Mathayo 25:45-46)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI *-Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** -Watu wote tutakwenda mbele za Mungu kutoa hesabu kwaajili ya maisha yetu. Kuishi maisha ya milele pamoja na Mungu itategemea uhusiano wetu na mungu.

# HUKUMU

*Yesu Kristo Atahukumu Watu Wote*

SOMO 4-11

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu alikuja duniani kuwarejeshea watu uhusiano wao na Mungu. Atarudi tena duniani kuzikomesha kazi zote za shetani na kuhukumu watu waovu, kuhukumu wale wote ambao hawakumpokea yeye kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yao. Yesu atawapa hesabu wenye haki kwa imani yao.

Andiko la msingi: *kwa sababu Bwana mwenyewe ashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kasha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili tumlaki Bwana hewani, na hivyo tutakuwa na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo (1 Thessalonike 4:16-18)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Katika hadithi hii Yesu alishasema kabla ya hukumu ijayo kuja kwa watu katika mwisho wa maisha duniani.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Maana kama Baba awafufuavyo wafu na kuwa huisha, vivyo hivyo na mwana awahuisha wale awatakao. Tena Baba hamhukumu mtu yeyote bali amempa mwana hukumu yote. Ili watu wote wamheshimu mwana kama vile wanavyomheshimu Baba aliyempeleka. Amini amini nawaambia yeye asikiaye neno langu, na kumwamini yeye aliyenipeleka, yuna uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bli amepita kutoka mautini, kuingia uzimani. Amin amin, nawaambia, saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakaposikia sauti ya mwana wa Mungu, na wale wasikiao watakuwa hai. Maana kama vila Baba alivyo na uzima nafsini mwake. Naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni mwana wa Adamu. Msistaajabie maneno hayo kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makabulini, wataisikia sauti yake. Nao watatoka waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima. Na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu. Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo na hukumu yangu ni ya haki, kwa sababu siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake yeye aliyenipeleka. (Yohana 5:21-30)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Ufunuo 20:11-15; Marko 9:41-48; 2 Korintho 5:10; 1 Korintho 3:11-15)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** - Yesu anatuonya kwamba, tungalikuwa tayari kwaajili ya yeye kurudi kuhukumu waovu na kuwapa thawabu wale walioishi kwa haki.

# MEZA YA BWANA

SOMO 4-12

*Umuhimu Wa Kukumbuka Kifo Cha Yesu Kristo Kwaajili ya Dhambi Zetu.*

## KIINI CHA SOMO - *Kuandaa Udongo*

Yesu aliwafundisha wafuasi wake washiriki meza ya Bwana mara kwa mara. Huu ni mfano halisi kivitendo uliofanyika kukumbuka kifo cha kujitoa dhabihu cha Yesu ambacho alilipa gharama kwaajili ya dhambi za watu.

Andiko la msingi: *Akautwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa akisema, huu ndio mwili wangu kwaajili yenu, fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Kikombe nacho vivyo, hivyo baada ya kula; akasema; kikombe hiki ni agano jipya katika damu yake, inayomwagika kwa ajili yenu.(Luka 22:19-20)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Usiku kabla ya kifo cha Yesu juu ya msalaba alishiriki chakula chake cha mwisho na wanafunzi wake. Wakati huu aliwahitaji wanafunzi wake wamkumbuke mara kwa mara, na kifo chake juu ya msalaba.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*lakini katika kuagiza haya, siwasifu ya kwamba, mnakusanyika, si kwa faida, bali kwa hasara, kwa maana kwanza mkutanikapo kanisani nasikia kuna faraka kwenu; name nusu nasadiki, kwamaana lazima kuwapo na uzushi kwenu, ili waliokubaliwa wawe dhahiri kwenu. Basi mkutanikapo pamoja haiwezekani kula chakula cha Bwana; kwa maana kila mmoja hutangulia kutwaa chakula chake katika kule kula, hata huyu ana njaa na huyu amelewa, Je! Hamna nyumba za kulia na kunywea? Au mnadharau kanisa la Mungu na kuwatahayarisha hao wasio na kitu? Niwaambieni nawasifu? La! Siwasifu kwaajili ya hayo kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa ninyi ya kuwa Bwana Yesu usiku aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru, aliumega, akasema, huu ndiyo mwili wangu, ulio kwaajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila muulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. (1 Korintho11:17-26)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(1 Korintho11:17-34; Luka 22:7-38; Yohana 6:47-58; Ufunuo 19:9)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** - Meza ya Bwana ni wakati wa kumheshimu Yesu na ni wakati ambapo tunaweza kuangalia maisha yetu kiundani kama yamekubalika na Mungu. Ni wakati ambapo wafuasi wa Kristo wangelimwabudu Bwana ambaye alijitoa mwenyewe kwa ajili ya watu wote.

# UBATIZO

*Kutangaza Mbele ya Watu*
*Juu ya Imani ya Kristo*

SOMO
4-13

## KIINI CHA SOMO -*Kuandaa Udongo*

Ubatito wa maji mengi ni muhimu sana kwa maisha ya mwamini mpya. Ubatizo ni wakati mwamini mpya anapofanya tangazo mbele za watu kwa imani yake katika Kristo, kwa kuzamishwa katika maji, kwa mfano wa mauti ya njia za zamani za maisha.

Andiko la msingi: *Peter replied, "Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake, Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38)*

## Simulizi Ya Biblia - *Kupanda Mbegu*

***Utangulizi unatoa habari ili kusaidia kufahamu simulizi.***

Yesu alikuwa na binamu aliyeitwa Yohana mbatizaji. Yohana mbatizaji alikuwa anawaambia watu, wabatizwe katika maji kama ishara ya toba kutoka katika dhambi zao. Yesu hakufanya dhambi, bali alijisikia kuwa ilikuwa ni muhimu kwenda kupitia mfano halisi kivitendo kuonyesha wengine mfano wa ubatizo.

***Simulizi ya Biblia inaanza hapa:-***

*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alimzuia akisema mimi nataka kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka mjini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akaja juu yake na tazama sauti kutoka mbinguni ikasema, huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye." (Matthew 3:13-17)*

## MCHAKATO wa UGUNDUZI - *Maji na rutubisha*

## MAANDIKO YA KUSOMA YA NYONGEZA - *Kupunguza*

*(Rumi 6:3-13; Mathayo 28:16-20; Korintho 2:9-12; Matendo 8:26-40)*

## MAOMBI NA MASWALI/MSINGI -*Kuvuna Matunda* *(2 Timotheo 3:16-17)*

**===HITIMISHO** - Agano jipya linatufundisha kuwa ubatizo wa maji mengi ni muhimu katika maisha waamini. Ubatizo wa maji mengihuonyesha ishara ya mauti yetu katika njia za zamani na maisha mapya katika Kristo.

*Wito Ili*

# Kuzaa Matunda na Kuongezeka

Katika uumbaji tumeona Mungu ameumba kila kitu kikiwa na uwezo wa "kuzaliana" na "kuongezeka." Biblia kuhusu uumbaji inaeleza kuwa viumbe vyote viliumbwa kwa kujizalisha vyenyewe 'kwa namna yake'; Mungu kamuumba mwanadamu kwa kanuni ya kuzaa matunda na kuongezeka, haikubadilika. "Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha" (Mwanzo 1:27-28).

Sisi ni wa kwanza kuumbwa na Mungu na kubarikiwa na Mungu kuzaa matunda na kuongezeka juu ya nchi. Kwa zaidi ya miaka 6,000 mwanadamu ametimiza ahadi hii na amejaza dunia.

Yesu alipokuwa akitembea dunia aliongea kuhusiana na mahitaji pamoja na kuzaliwa mara ya pili au kuzaliwa kiroho. Kiukweli Yesu alisema, mtu hataingia Ufalme wa Mungu bila kuzaliwa mara ya pili. Yesu akajibu, "Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho" (Yohana 3:5-6).

Kristo ametuita kwenye maisha mapya. Haya maisha mapya hutolewa na Roho Mtakatifu. Sisi tunaadhimisha maisha mapya kwa kubatiza katika maji. Amri ya Kristo ya kuzaa matunda na kuongezeka hufanyika kwa kuzaliwa mara ya pili na Roho Mtakatifu. Katika maisha mapya ndani ya Kristo tumepewa upendeleo na amri ya kuwa na maisha mapya ya kiroho. "Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatuifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.'" (Mathayo 28:18-20)

Tumeitwa na Kristo kuwabatiza na kuwaingiza watu ndani ya ufalme wa Mungu. Tumeitwa kuisha maisha yenye kuzaa matunda, yatakayopelekea kuzaliana Kiroho. Mtaala wa BFAM umeandaliwa ili kuwafanya wanafunzi wa Yesu Kristo na kuwaongoza katika maisha ya kuzaliana Kiroho yenye kuleta tokeo la maongezeko. "Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele (1 Petro 1:23).

Bwana na awabariki kwa matunda tele na kuzaa na kuongezeka kiroho katika maisha na huduma. Na tuone dunia hii ikiwa imejaa watu waliozaliwa mara ya pili katika ufalme wa Mungu!

| | |
|---|---|
| Kwa mawasiliano na Ofisi ya Every Home for Christ katika Eneo lako:<br><br>(Ingiza anwani ya ofisi yako kwenye taifa lako) | Imetolewa na Every Home for Christ kwa ushirikiano na:<br><br>(Ingiza jina la huduma yako hapa) |

Every Home for Christ International
P.O. Box 64000, Colorado Springs, CO 80962-4000
www.iBFAM.org
*Version 4.0*